Haliuzwi
JANUARI 6, 2026
/islamicftz
Rajab 17 1447
# IMAAN
ISSN 5618 - NO. 565
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Dunia yachukizwa jaribio la ukoloni la Marekani Venezuela




# Serikali yatambua mchango wa Uislamu katika ujenzi wa amani

## Wadau wapongeza kanuni za benki bila riba lakini...

## Meya Morogoro: The Islamic Foundation mshirika muhimu wa maendeleo



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Khalid Matengo akiwa na Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi katika ziara ya kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi hiyo katika kuwahudumia wananchi.



## TMA yatangaza mvua za siku 10 mfululizo

## Rais Samia: Tuzo ya utalii ni matokeo ya uhifadhi, mshikamano



## Tanzania ijifunze kwa nchi za Kiarabu kunufaika na maji ya bahari

## Matumaini tele Mwinyi akizindua flyover ya kwanza Zanzibar



## Ripoti: Waislamu Uingereza wakarimu mara nne zaidi

NA YUSUFU AMINI

# Hatimaye kanuni za benki zisizotoza riba zatoka, wadau wapongeza

Wadau na wasomi waliobobea katika masuala ya huduma za kibenki za Kiislamu wamepongeza kanuni za kuendesha huduma hiyo zilizotangazwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwenye Gazeti la Serikali la Desemba 19, 2025.

Wadau na wasomi hao wameeleza kuwa kanuni hizo zina tija kubwa hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya huduma za benki zinazofuata mfumo wa Kiislamu yanazidi kuongezeka siku hadi siku. Wamesema kanuni hizo zitasaidia watu na taasisi zinazofuata misingi ya sheria za Kiislamu kutoa/kupata huduma za kifedha kwa urahisi bila kutofautiana na sheria za nchi.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Gazeti Imaan, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirkah Asset Managemnent, Salum Awadh, licha ya kupongeza alisema bado ipo haja ya kuangalia mapungufu yaliyopo katika kanuni hizo na kuyafanyia kazi.

"Ni hatua nzuri kuelekea kuwa na mfumo wa kisheria maalum kwa ajili ya benki na huduma za kifedha za kiislam ila kanuni hizi bado zinatakiwa kuangaliwa tena, kupitia mapungufu, na kuzifanya ziwe kweli jibu kwa hitajio."

Aliongeza: "Ni muhimu benki kuu ikakaa na taasisi kama CIFCA, kama mwakilishi wa sekta ya fedha ya kiislam, na kupitia mapunfufu yaliyopo."

Naye Mwenyekiti Mtendaji Yusra Sukuk Co Ltd, Sheikh Mohammed Issa, amesema kutangazwa kwa kanuni hizo ni hatua kubwa katika mfumo wa fedha wa Kiislamu hapa nchini kwani hapo awali hakukuwa na sheria rasmi inayosimamia miamala ya kifedha ya Kiislamu katika benki za Kiislamu.

Hata hivyo, Sheikh Issa alisema bado benki zitahitaji miongozi (guidelines) itakayofafanua kanuni kwa undani zaidi.

"Tumeridhika na kanuni hizi ingawa tunategemea kwamba Benki Kuu itatoa miongozo (guidelines) kwa benki zinazofuata mfumo wa kifedha wa Kiislamu, kama ambavyo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) ilitoa miongozo ya Takaful," alieleza Sheikh Issa.

Sheikh Issa alifafanua kuwa 'regulations' au kanuni pekee haziwezi kukidhi matakwa au mahitajio ya huduma za kibenki za mfumo wa fedha wa Kiislamu kwani zenyewe huwa ni fupi mno na hazitaji mambo kwa urefu.

## Asifu ushirikishwaji

Sheikh Issa alibainisha kuwa, wao kama wadau muhimu wa sekta ya mfumo wa fedha wa Kiislamu walishirikishwa kuandaa miongozo hiyo kwa muda wa takriban miaka mitano, ambapo wamefanikiwa kutatua matatizo mengi ambayo yalikuwa yanazikabili benki zinazofuata mfumo wa fedha wa Kiislamu.

Zaidi, Sheikh Issa aliishukuru Benki Kuu ya Tanzania kwa kufikia hatua hii muhimu katika sekta ya kifedha ya Kiislamu, kwa sababu Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo huduma za kifedha za Kiislamu zilikuwa zinatolewa bila kuwa na sheria yoyote inayozisimamia.



"Kwa kweli ni hatua muhimu sana na tunampongeza Gavana na timu nzima ya watendaji wa Benki Kuu," alieleza Sheikh Issa na kusema kuwa iwapo BOT watatoa miongozo kama ambavyo waliiandaa kwa kushirikiana nao, basi itakuwa inakidhi mahitaji yao.

## Kanuni kwa ufupi

Kanuni hizi zimewekwa ili kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za benki zinazozingatia misingi ya Shariah nchini Tanzania, zikihusu benki zote zinazotoa huduma za kifedha zisizohusisha riba, iwe ni benki za Kiislamu kamili au benki za kawaida zilizoanzisha madirisha maalum ya benki isiyo na riba.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, lengo kuu ni kuhakikisha kuwa huduma hizo zinaendeshwa kwa uwazi, uadilifu na kwa kuzingatia sheria za Kiislamu.

Muongozo huo unaeleza masharti ya kuanzisha benki isiyo na riba au dirisha la benki ya Kiislamu, ikiwemo kupata vibali kutoka Benki Kuu, kuwasilisha tafiti za uwezekano wa biashara, pamoja na kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa Shariah. Aidha, unasisitiza ulazima wa kutenganisha kabisa fedha na kumbukumbu za biashara ya Kiislamu na zile za benki za riba ili kuzuia kuchanganywa kwa miamala inayokatazwa na Shariah.

Kanuni hizo pia zinaweka wazi muundo wa uongozi wa benki zisizo na riba, ikiwemo wajibu wa bodi za wakurugenzi na kuanzishwa kwa Kamati za Ushauri wa Shariah. Kamati hizo zinapewa mamlaka ya kushauri juu ya uhalali wa bidhaa za kifedha, kukagua miamala, kusimamia ukaguzi wa Shariah, na kuhakikisha kuwa mapato yoyote yasiyokubalika kwa misingi ya Kiislamu yanatambuliwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa kanuni.

رَجَب

HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

# Rais Samia: Tuzo ya utalii ni matokeo ya uhifadhi, mshikamano




Rais Samia Suluhu Hassan, amesema mafanikio ya Tanzania kuendelea kutwaa Tuzo za Kimataifa za Utalii yanatokana na uwekezaji wa muda katika uhifandhi wa rasilimali asilia, mshikamano wa wadau na juhudi za makusudi za kuitangaza nchi Kimataifa

Amesema ushindi huo si wa bahati, bali ni matokeo ya kazi endelevu inayofanywa na taasisi za Serikali, sekta binafsi na jamii kwa ujumla

Tuzo hizo ziliwasilishwa kwake na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk Ashatu Kijaji.



MWANDISHI WETU



# Matumaini tele Mwinyi akizindua flyover ya kwanza Zanzaibar

Msongamano wa muda mrefu wa magari na ucheleweshaji katika makutano yenye shughuli nyingi ya barabara ya Mwanakwerekwe hatimaye umepungua kufuatia uzinduzi wa flyover ya kwanza Zanzibar katika eneo hilo.

Makutano hayo yanaunganisha barabara zinazoelekea uwanja wa ndege hadi Amani na Fuoni kwenda katikati ya jiji. Maafisa wanasema ufunguzi wa flyover hiyo hautapunguza tu msongamano wa magari bali pia utachochea na kuimarisha shughuli za kiuchumi visiwani.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi jana, Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, alisema kuwa katika kipindi cha miaka 62 tangu Mapinduzi ya Zanzibar, visiwa hivyo vimepiga hatua kubwa za maendeleo, ikiwemo kuandika historia kwa kujenga flyover kwa mara ya kwanza ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Huu ni mradi wa kimkakati unaolenga kupunguza msongamano wa magari, kuboresha usalama barabarani na kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo uliopewa jina la Flyover ya Hussein Ali Hassan Mwinyi Mwanakwerekwe ni matokeo ya uwekezaji mkubwa



wa serikali katika miundombinu, akieleza kuwa miundombinu bora ni nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi, kuvutia uwekezaji na kuongeza shughuli za biashara.

"Kaulimbiu yetu ni uongozi unaoacha alama. Leo tumeitekeleza ahadi hiyo kwa vitendo, na hizi ndizo alama tunazozizungumza," alisema.

Dk Mwinyi alisema serikali itaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ili kuboresha ustawi wa wananchi na kuinua uchumi wa Zanzibar kwa ujumla.

Aidha, alionya dhidi ya uvamizi wa hifadhi za barabara, akieleza kuwa serikali inapanga kufunga miundombinu ya maji, umeme, mawasiliano na njia za waenda kwa miguu, hivyo si busara kujenga katika maeneo hayo. Dk Mwinyi aliipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi yake ya ujenzi wa barabara katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba, akisema ameridhishwa na utendaji wake licha ya kuwa na majukumu mawili ya ujenzi na uchukuzi.

Pia aliipongeza Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa kutekeleza miradi ya barabara kwa viwango bora na kwa kuzingatia muda uliokubaliwa.

Awali, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk Khalid Salum Mohammed, alisema mafanikio yanayoonekana yanaakisi maono na uongozi wa Rais katika kutekeleza mipango na ahadi zake za mwaka 2020, ikiwemo kuimarisha mtandao mzima wa barabara za mijini na vijijini na kuboresha barabara kwa viwango vya lami bora Unguja na Pemba.

Dk Khalid alisema Rais Mwinyi pia aliahidi kujenga flyover mbili ili kupunguza msongamano wa magari, ahadi ambayo sasa imetekelezwa, na kuacha urithi wa kudumu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

NA YUSUFU AMINI



# Meya Morogoro: The Islamic Foundation ni mshirika muhimu wa maendeleo

Katika hatua inayodhihirisha dhamira ya serikali za mitaa kushirikiana na taasisi za kijamii katika kuleta maendeleo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Khalid Matengo, ameahidi kutoa ushirikiano wa karibu kwa Taasisi ya The Islamic Foundation, akibainisha mchango wake mkubwa katika maendeleo ya jamii.

Ahadi hiyo imetolewa wakati wa ziara maalum aliyoifanya Meya Matengo katika makao makuu ya Taasisi ya The Islamic Foundation yaliyopo ndani ya Manispaa ya Morogoro, ambapo alipokelewa na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Aref Nahdi, pamoja na viongozi wengine.

Ziara hiyo ilimuwezesha Meya kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi hiyo katika kuwahudumia wananchi, hususan katika masuala ya kiimani kupitia ujenzi wa misikiti, pamoja na ustawi wa jamii kupitia vyombo vya habari vya Imaan na miradi ya uchimbaji wa visima vya maji.



Akizungumza na Dira ya Habari mara baada ya ziara hiyo, Meya Matengo alisema The Islamic Foundation imekuwa mshirika muhimu wa maendeleo kwa kushiriki katika miradi inayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi wa Morogoro.

Alisisitiza kuwa serikali ya manispaa itaendelea kushirikiana na taasisi hiyo ili kuhakikisha jitihada zinazofanywa zinakuwa na tija zaidi kwa jamii ya Morogoro.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, alimshukuru Meya kwa kutembelea taasisi hiyo na kuonesha utayari wa kushirikiana, akieleza kuwa ushirikiano kati ya serikali na taasisi za kijamii ni msingi muhimu wa kuleta maendeleo endelevu na kujenga jamii yenye mshikamano. Ziara hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano ambao umekuwa ukileta matokeo chanya kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro, na huku pia ukiimarisha nafasi ya taasisi za kijamii katika kuchangia maendeleo ya taifa kwa ujumla.

MWANDISHI WETU

# TMA yatangaza mvua za siku 10 mfululizo



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeonya kuwapo kwa mvua kubwa na radi kwa kipindi cha kuanzia Januari mosi hadi 10, 2026, huku vipindi vya mvua chache vikitarajiwa katika baadhi ya maeneo ya Tanzania.

Kwa mujibu wa TMA, mikoa inayotajwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi ni ile ya Kanda ya Ziwa ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara. Kwa upande wa Nyanda za Juu Kaskazini – Mashariki, mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro itapata vipindi vya mvua chache, hasa katika siku tano za mwanzo za Januari.

Pwani ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Tanga, maeneo ya Kaskazini mwa Morogoro, Pwani ya Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, pia vinatarajiwa kupata mvua.

Aidha, mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora inatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo katika kanda ya Magharibi mwa nchi, huku Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma na Singida ikitarajiwa kupata mvua zinazoambatana na radi, hususan siku tano za mwanzo za Januari.

Kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini – Magharibi, mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa inatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo, wakati mikoa ya Pwani ya Kusini ya Mtwara na Lindi, kulingana na taarifa ya TMA, itapata vipindi vya mvua chache.

NA YUSUFU AMINI



# Nahdi ausia madiwani uadilifu, uchapakazi

> "Nyie ni viongozi mliopatikana kwa kuchaguliwa na wananchi, ikiwa ni mhimili wa kusaidia jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan katika kujenga taifa katika maeneo yenu"
> **Aref Nahdi**

Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, aliwataka madiwani kuendelea kuwa waadilifu na wachapakazi ili ili kuendelea kupata imani ya wananchi katika chaguzi zijazo na kusukuma mbele mipango ya maendeleo ya serikali ya Awamu ya Sita.

Nahdi alitoa rai hiyo wakati akiwapokea madiwani kutoka Wilaya ya Kondoa Mjini mkoani Dodoma walipotembelea ofisi za taasisi hiyo kujionea namna inavyoendesha shughuli zake, hususan miradi ya kidini na kusaidia jamii.

"Nyie ni viongozi mliopatikana kwa kuchaguliwa na wananchi, ikiwa ni mhimili wa kusaidia jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan katika kujenga taifa katika maeneo yenu," alisema Nahdi.

Aliongeza kuwa jukumu kubwa la madiwani ni kuimarisha ustawi wa jamii na kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.

Moja ya idara muhimu ambazo madiwani hao walitembelea ni Kituo cha Matangazo cha Redio na Televisheni ya Imaan.

Kwa upande wao, madiwani hao walipongeza taasisi ya The Islamic Foundation kwa mchango wake katika maendeleo ya jamii, ikiwemo uchimbaji wa visima, ujenzi wa misikiti na utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari.

Madiwani hao walisema The Islamic Foundation ni miongoni mwa taasisi zinazopaswa kuigwa kutokana na utoaji wake wa huduma za kijamii bila ubaguzi, hatua inayolenga kurejesha matumaini kwa wananchi wenye uhitaji.

Diwani wa Kata ya Kondoa Mjini, Said Ndwata, alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa mchango mkubwa kiasi cha madiwani kushuhudia moja kwa moja matunda ya miradi yake.

"Vipindi vyao vinahamasisha amani nchini, lakini pia wanatoa misaada ambayo hata serikali bado haijafika, ikiwemo ujenzi wa misikiti na shule," alisema Ndwata.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Salum Hassan Mabote, alisema taasisi hiyo ni mdau mkubwa wa maendeleo, akibainisha kuwa katika kata yake wamepata visima viwili na msikiti.

Naye Katibu wa Taasisi hiyo, Mussa Buluki, alisema mahusiano mazuri kati ya taasisi hiyo na Wilaya ya Kondoa yameiwezesha The Islamic Foundation kujenga jumla ya visima 16 ndani ya wilaya hiyo.

# MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Nyamguma Mahmud

## Serikali yatambua mchango wa Uislamu katika ujenzi wa amani

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Athumani Mtambule amesema Serikali inatambua mchango wa Uislamu katika ujenzi wa amani ya nchi.

Saad amesema hayo wakati akihutubia hadhara katika kongamano la nne la Misk ya Roho, lililofanyika katika Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, DC Mtambule alipongeza jitihada za The Islamic Foundation kwa kuandaa kongamano hili na kujikita katika mada nyeti na muhimu katika kipindi hiki muhimu.

DC Mtambule alionyesha nafasi muhimu ya dini ya Kiislamu na mafundisho ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) katika kukuza amani na mshikamano wa kijamii. Akisisitiza kuwa dini ya Uislamu inatufundisha kuheshimiana, kutimiza haki za kila mtu, na kuishi kwa amani, jambo ambalo ni msingi wa mshikamano wa familia na jamii.

Mkuu wa Wilaya pia ameunga mkono juhudi za The Islamic Foundation za kuhamasisha amani. "Kama nchi ambayo inaendelea, suala la amani ni msingi wa maendeleo chanya tunayaoyalenga," alisema DC Mtambule

DC Mtambule alihimiza wananchi kuelewa misingi ya amani na kuwa haiwezi kusimama bila msingi wa ushirikishwaji wa jamii.

Akichangia mjadala wa ni misingi ya amani, alihoji: "Je, amani chakula chake ni kipi? Haki, demokrasia au huduma za kijamii? Lakini yote yanategemea muktadha na mazingira husika." alieleza DC Mtambule.

"Kuna haja ya kuilinda hii amani tuliyonayo na kuhuisha amani tunayohitaji katika jamii zetu," amesiema DC Mtambule akiongeza kuwa amani ni jukumu la kila raia na kila sekta inapaswa kuchangia katika kudumisha utulivu na mshikamano wa kijamii.

DC Mtambule amebainisha kuwa amani ni sehemu muhimu ya maendeleo endelevu na inapaswa kuimarishwa na viongozi wa dini na serikali kwa kushirikiana. Akieleza kuwa matokeo ya amani yanapoongezwa katika familia, shule, na jamii, hupelekea maendeleo ya kila sekta ya maisha ya wananchi.

Kongamano la Miski ya Roho limekuwa jukwaa la waumini wa Kiislamu kujifunza na kuhuisha maadili katika jamii. Mada zilizojadiliwa mwaka huu 2025, ikiwemo hotuba ya DC Mtambule, zimeakisi misingi ya mafundisho ya Kiislamu na maisha ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kama dira ya kuimarisha mshikamano, heshima, haki, na ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.



## Mufti alivyoisifu The Islamic Foundation katika Misk ya Roho

Mufti wa Tanzania, Sheikh Dkt. Abubakar Zubeir bin Ally amezitaka taasisi za Kiislamu kuiga mfano wa taasisi ya The Islamic Foundation (TIF) katika kuandaa makongamano yenye lengo la kuhamasisha jamii kuithamini amani iliyopo nchini.

Mufti Zuberi ametoa wito huo katika khutba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Mufti, Sheikh Ally Ngeruko alipomwakilisha katika Kongamano la Misk ya Roho, lililofanyika kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee Jumamosi iliyopita.

Katika khutba hiyo, Sheikh Ngeruko amezitaka taasisi nyingine za Kiislamu kuandaa makongamano kwa ajili ya kutathmini njia bunifu za kulinda na kudumisha amani.

"Elimu ni ngao bora, hekima ni nuru bora; hujenga jamii bora, hufunza njia sahihi. Hivyo tukiwa kama viongozi lazima tusimame kuelimisha umma kwa juhudi zote,... tuendeleze haya makongamano yawe mengi katika nchi yetu hii siku hadi siku ili tutoke katika mawindi haya ya fitina, tuweze kukabiliana nayo kwa hekima, kwa subira na amani kama sasa tunavyokabiliana nayo," alieleza Sheikh Ngeruko.

Kuhusu mada zilizowasilishwa katika kongamano hilo, Sheikh Ngeruko aliwataka Waislamu kuzitafakari na kuziishi. "Mheshimiwa Mufti ametoa wito wa kuzitafakari mada zinazitolewa hapa. Na kama kuna uwezekano mtu awe ananukuu na kutafuta rejea ili kuzisherehesha zaidi kila pointi na kila eneo linalozungumzwa na mzungumzaji.

"Kongamano (la mwaka huu) limependeza sana kutokana na uwasilishaji wa mada ya amani kwa wawasilishiji wa siku ysa leo. Wawasilishaji wetu Maasha Allah, kusema kweli hakuna haja ya kuzidisha jambo zaidi ya kuziishi mada zilizotolewa hapa na kuzitafakari," aliongeza kusema.

## Sheikh Abdulkhaliq: Amani inapatikana kwa mazungumzo, si vurugu

Katika zama hizi ambazo umma wa Kiislamu unakabiliwa na changamoto lukuki za kijamii, Sira (Historia) ya Mtume Muhammad inatazamwa kama kielelezo cha kufaulu kwa umma kutokana na mafundisho yake na matendo yake.

Hayo yamebainishwa na Sheikh Abdulkhaliq Issa kutoka Kenya wakati wa Kongamano la Misk ya Roho lililofanyika Jumamosi iliyopita katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

Sheikh Abdulkhaliq aliukumbusha umma wa Waislamu kuishi kwa kumfuata Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani iwe juu yake), akisisitiza kuwa Mtume alikuwa akiufikiria umma wake kuliko jambo lolote katika maisha yake.

Akizungumza na hadhira ya kongamano hilo, Sheikh Abdulkhaliq alirejea simulizi ya mama wa Waumini, Aisha (Allah amridhie), aliyesimulia kuwa alipomwona Mtume akiwa na furaha alimwomba amuombee dua, nae akafanya hivyo.

"Mtume aliinua mikono yake na kumuomba Allah amsamehe Aisha madhambi yake yote yaliyopita na yajayo, ya siri na ya wazi, na amuingize Peponi bila hesabu," alieleza Sheikh Abdulkhaliq na kuongeza kuwa, furaha aliyopata Aisha kutokana na dua hiyo ilimfanya Mtume aseme kuwa dua kama hiyo ndiyo ambayo huwaombea watu wa umma wake katika kila kipindi cha sala.

Katika maelezo yake, Sheikh Abdulkhaliq alihoji kwa huzuni na tafakuri, ikiwa Mtume alikuwa akiufikiria umma wake katika kila sala, basi ni mara ngapi Waislamu wa leo humkumbuka Mtume wao kwa vitendo, kwa kuziishi Sunna zake na kuonesha mapenzi ya kweli kwake.

Alisisitiza kuwa, mapenzi ya Mtume hayakuwa ya maneno tu bali yalijidhihirisha katika huruma, subira na msamaha wake kwa watu wote. Akifafanua zaidi, Sheikh Abdulkhaliq alieleza namna Mtume alivyofukuzwa katika mji wa Makka, lakini aliporejea kwa mara nyingine hakulipiza kisasi licha ya kutendewa uovu na kudhulumiwa.

MEDIA PARTNER'S 2025
azam media, azam tv, 2BC2, DUA tv, AL-HAAJAR TV, tvImaan Tanzania, Radio Imaan FM, IMAAN NEWSPAPER, IMAAN DIGITAL

MWANDISHI WETU

# Mwinyi: SMZ kuendelea kujenga masoko ya kisasa katika kuimarisha biashara Z'bar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaendelea na ujenzi wa masoko ya kisasa katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika mazingira bora, salama na yenye hadhi. Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo leo tarehe 4 Januari, 2026 alipolizindua Soko la Kisasa la Mbogamboga la Mombasa, lililopo Mkoa wa Mjini Magharibi.

Ameeleza kuwa Serikali inapowahamisha wafanyabiashara kutoka maeneo yao ya awali, hufanya hivyo kwa nia njema ya kujenga masoko yenye viwango na hadhi, pamoja na kuwaandalia mazingira mazuri yatakayochangia ukuaji wa biashara zao na ustawi wa maisha yao.

Rais Dkt. Mwinyi amewahakikishia wananchi kuwa Serikali ipo katika maandalizi ya kujenga soko kubwa na la kisasa katika eneo la Kibanda Maiti, pamoja na uanzishaji wa Bazaar katika Mtaa wa Kwa Hajitumbo, Wilaya ya Mjini, hatua itakayosaidia kudhibiti biashara holela, kuondoa mazingira duni katika masoko na kuzuia ufanyaji wa biashara pembezoni mwa barabara.

Aidha, amesema Serikali itaendelea kutoa mikopo isiyo na riba kwa wafanyabiashara ili kuwawezesha kukuza mitaji yao, huku akitoa wito kwa watakaopewa fursa ya kuliendesha soko hilo jipya kuhakikisha wanalinda miundombinu na kuimarisha usafi wakati wote.

Rais Dkt. Mwinyi ametoa maelekezo maalum kwamba wafanyabiashara wa mwanzo waliopisha ujenzi wa Soko la Mombasa wapewe kipaumbele wakati wa ugawaji wa vizimba vya kufanyia biashara sokoni hapo.

Vilevile, ameushauri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kujikita zaidi katika uwekezaji wa miradi mikubwa yenye tija, ikiwemo nishati ya umeme, teksi za baharini na mabasi ya umeme, kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika miradi ya nyumba za Makaazi na Masoko.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Ndugu Nassor Shaaban, ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuiamini taasisi hiyo katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji inayochangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Zanzibar, ikiwemo ujenzi wa nyumba za Makaazi na Masoko ya kisasa.



**MAKALA**
**MAALUM**

Na Said Rajab
0783 650 803

# Fadhila na ubora wa Miezi Mitakatifu



**Miongoni mwa ukamilifu wa kumtukuza Allah Mtukufu ni kukitukuza kila alichokifanya kuwa kitukufu miongoni mwa alama za dini na ibada. Miongoni mwa utukuzaji huo ni kuitukuza miezi Mitakatifu aliyoipa heshima maalumu, ambayo ni Dhul–Qa'ada, (Mfungo pili), Dhul–Hijja (Mfungo tatu), Muharram (Mfungo nne) na mwezi huu wa Rajab.**

# Fadhila na ubora wa Miezi Mitakatifu

Miongoni mwa ukamilifu wa kumtukuza Allah Mtukufu ni kukitukuza kila alichokifanya kuwa kitukufu miongoni mwa alama za dini na ibada. Miongoni mwa utukuzaji huo ni kuitukuza miezi Mitakatifu aliyoipa heshima maalumu, ambayo ni Dhul–Qa'ada, (Mfungo pili), Dhul–Hijja (Mfungo tatu), Muharram (Mfungo nne) na mwezi huu wa Rajab.

Allah Mtukufu anasema: "Hakika idadi ya miezi mbele ya Mwenyezi Mungu ni kumi na miwili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu, tangu siku alipoumba mbingu na ardhi. Miongoni mwa miezi hiyo (kumi na miwili), minne ni Mitakatifu..." [Qur'an, 9:36].

Kadhalika, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Hakika wakati umerejea katika hali yake ya awali, tangu siku Allah alipoumba mbingu na ardhi. Mwaka una miezi kumi na miwili; minne miongoni mwa hiyo ni Mitakatifu, mitatu imefuatana, nayo ni Dhul–Qa'ada, Dhul–Hijja na Muharram, mwingine ni Rajab..." [Bukhari na Muslim].

Wanazuoni wamejitahidi kubainisha hekima ya kutukuzwa miezi hii na siri ya kupangwa kwake kwa mpangilio huo. Ibn Kathir (Allah amrehemu) amesema: "Kwa hakika miezi Mitakatifu imefanywa minne; mitatu imetajwa mfululizo na mmoja peke yake, kwa ajili ya kutekeleza ibada za Hijja na Umra. Mwezi wa Dhul–Qa'ada umekuwa Mtakatifu kwa sababu watu huacha mapigano ndani yake, na utukufu wa mwezi wa Dhul–Hijja ni kutokana na watu kushughulika na utekelezaji wa ibada ya Hijja.

"Mwezi wa Muharram umekuwa Mtakatifu kwa sababu watu (mahujaji) hurudi katika maeneo yao ya mbali wakiwa salama; na utukufu wa mwezi wa Rajab, ulio katikati ya mwaka ni kwa ajili ya kuizuru Nyumba Tukufu ya Allah (Al–Ka'aba) na kufanya ibada ya Umra kwa wale wanaokuja kutoka maeneo ya mbali ya Bara Arabu, wazuru kisha warudi kwao wakiwa salama."

Nae Imam Ibn Ashura (Allah amrehemu) ameeleza kuwa, utukufu wa miezi hii ni miongoni mwa sharia walizowekewa watu tangu zama za Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) kwa ajili ya maslahi ya watu na kusimamisha ibada ya Hijja. Allah anasema: "Mwenyezi Mungu ameifanya Al–Ka'aba (Nyumba Tukufu) kuwa kiini cha manufaa na tegemeo la watu, na (ameifanya) miezi Mitakatifu (kuwa ni sababu ya amani)..." [Qur'an, 5:97].

## Utukufu wa mwezi wa Rajab

Imepokewa kwamba, Mtume wa Allah kila uingiapo mwezi wa Rajab alikuwa akisema: "Ewe Allah, tubariki katika mwezi wa Rajab na Shaaban, na utuafikishe katika mwezi wa Ramadhan." Lakini mwanazuoni Ibn Taymiyyah (Allah amrehemu), baada ya kuitaja hadith hii amesema: "Haikuthibiti kutoka kwa Mtume wa Allah hadith yoyote nyingine kuhusu fadhila za mwezi wa Rajab, bali hadith zote zilizopokelewa kuhusu hilo kutoka kwa Mtume ni za kubuniwa (si sahihi)."

Hakika wazushi wamebuni hadith nyingi kuhusu fadhila za mwezi huu Mtakatifu (Rajab) pamoja na kuuhusisha na baadhi ya ibada maalumu, kama vile sala na kufunga.

Miongoni mwa waliobainisha jambo hili ni mwananzuoni nguli wa fani ya hadith katika madhehebu ya Shafi, Ibn Hajar, ambaye amesema: "Haikupokelewa hadith yoyote sahihi inayoweza kuwa hoja kuhusu fadhila ya mwezi wa Rajab, wala kuhusu kufunga mwezi wote, wala kufunga siku maalumu ndani yake, wala kusimama kwa ibada (Qiyam) katika usiku maalumu."

Kisha Ibn Hajar akasema, kiujumla hadith zote zilizopokelewa kuhusu jambo hilo ni dhaifu, na akabainisha hukumu yake juu ya hadith hizo katika risala yake iitwayo "Tabyiin Al'ajab bimaa warada fii Fadhli Rajab".


Nae mwanazuoni Ibn Rajab (Allah amrehemu) amesema: "Haikuthibiti hadith yoyote kuhusu fadhila ya kufunga mwezi wa Rajab, si kutoka kwa Mtume wala Masahaba wake." Ni kwa sababu hiyo, wengi katika wema waliotangulia walichukia kuutenga mwezi wa Rajab kwa kuufunga.

Abubakr At–Turtushi amelifafanua hili kwa kusema kwamba, kuchukia kufunga ndani ya mwezi wa Rajab kuna sababu nyingi. Miongoni mwazo ni; mosi, ikiwa Waislamu watazoea kufunga ndani yake kila mwaka, watu wa kawaida wanaweza kudhani kuwa kufunga mwezi wa Rajab ni faradhi kama ilivyo kwa mwezi wa Ramadhan.

Pili, watu wanaweza kudhani kuwa kufunga katika mwezi huu ni Sunna iliyo thabiti na yenye fadhila maalumu kuliko miezi mingine, ilhali hilo halijathibiti. At–Turtushi ameendelea kusema kuwa, lau mwezi huu ungekuwa una fadhila maalumu, Mtume wa Allah angeufunga, au angeamrisha Masahaba wake kufunga. Kwa hiyo, kufunga mwezi huu si faradhi wala sunna, kwa makubaliano ya wanazuoni.

Kisha At–Turtushi akabainisha kuwa, ikiwa mtu atafunga ndani ya mwezi huo kwa nia ya kujizoesha (kuidhibiti) nafsi na akaweza kuzuia njia za kueneza kwa watu dhana potofu kuwa kufunga katika mwezi wa Rajab ni faradhi au sunna maalum, katika hali hiyo hakuna ubaya kufanya hivyo.

Ama kutekeleza ibada ya Umra ndani ya mwezi wa Rajab, wengi katika wema waliotangulia, akiwamo Khalifa Umar bin Khattwab na Mama wa Waumini, Aisha (Allah awaridhie wote) wamesema kuwa ni jambo linalopendelewa (mustahab).



رَجَب

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Kushawishi watoto wafeli ni kuua ndoto zao

Tumesikia simulizi za baadhi ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba mwaka jana wakisema walishawishiwa na wazazi wao kufanya vibaya katika mitihani ya taifa ili wasipate nafasi ya kwenda sekondari na badala yake wafanye kazi za kilimo au kuchunga mifugo.

Aidha, imeripotiwa kwa nyakati tofauti kwamba baadhi ya wazazi huwaoza watoto wao wa kike waliohitimu darasa la saba ikiwa ni mkakati wa kukimbia majukumu au kujipunguzia masuulia. Mbali na hao, pia kuna wanaothubutu kuozesha watoto wao kwa kisingizio cha kukosa fedha za kuwasomesha au pia kwa madai ya kuhuisha mila na desturi za jamii zao.

"Kuna mwenzetu mmoja alikuwa na akili sana darasani lakini matokeo yalipotoka hakufaulu kujiunga na sekondari, tulipomuuliza kulikoni alisema mama yake alimwambia aandike 0000 ili afeli na aolewe," alisema mmoja wa wanafunzi wa darasa la saba katika mojawapo ya shule zilizopo mkoani Tanga.

Mwanafunzi mwingine amesema, walisikia baadhi ya wazazi wakizungumza, "Bora mtoto afeli, mimi sina hela za kumhudumia atakapoingia sekondari." Si rahisi kuyaamini haya lakini hiyo ndiyo hali halisi iliyopo katika maeneo mengi nchini.

Kadhalika, imebainika baadhi ya wazazi na walezi wanawahonga fedha au mifugo maofisa watendaji na wakati mwingine walimu wakuu ili watoto wao waliofaulu kuingia kidato cha kwanza wasiendelee na masomo ili wachunge mifugo ama kuolewa. Ni kweli kabisa kuwa ndoa ni muhimu kwa mabinti, lakini elimu pia ni muhimu hasa katika umri huo mdogo.

Tunawashauri wazazi na walezi ambao bado wana mawazo mgando kuwa mtoto wa kike ni wa kuolewa tu, waachane na fikra hizo kwani watoto wa kike nao wanapaswa kulindwa na kupatiwa fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari kama ilivyo kwa watoto wa kiume.

Sambamba na hivyo, pia tunawahimiza wazazi na walezi waendeleze jukumu la kuwanasihi watoto wao juu ya kudumisha tabia njema. Tunasema hivyo kwa sababu, mara kwa mara tumekuwa tukisikia baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wakifanya vitendo viovu vya uvutaji sigara na bangi, kucheza kamari na wizi.

Lililo muhimu kwa wazazi ni kuhakikisha wanaendelea kusimamia tabia njema za watoto wao walizofunzwa na walimu wao. Mwisho, tunawaombea heri na baraka walezi na wazazi wote waliopeleka watoto wao shuleni, kwani suala la kujifunza ni nyeti na muhimu kwenye maisha ya mwanadamu.

Mwenyezi Mungu anasema: "Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, na akasema, 'Niambieni majina ya hivi ikiwa mnasema kweli.' Wakasema, 'Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa kwa uliyotufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye Hekima.' Akasema, 'Ewe Adam! Waambie majina yake.' Basi alipowaambia majina yake, (Mwenyezi Mungu) alisema: "Sikukwambieni kwamba Mimi ninajua siri za mbinguni na za duniani, na ninayajua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha?" [Qur'an, 2:31–33].



رَجَب




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

**Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amewapongeza vijana wa kujitolea wa Taasisi hiyo kwa kazi ya dhati waliyoifanya katika kambi ya matibabu ya macho bila malipo iliyofanyika Mkoani Morogoro.**

**Mwenyekiti Aref Nahdi ametoa pongezi hizo wakati wa hafla fupi ya utoaji wa vyeti kwa washiriki wa kujitolea waliotoa huduma katika kambi hiyo, akisema vijana hao walihudumia wananchi kwa moyo safi, hali iliyoleta faraja kubwa kwa jamii iliyohudumiwa.**






















MAKALA MAALUM

SHEIKH Shaaban Mussa 0786 272 323

# Ahlu Sunnah ni nani? Ufafanuzi wa kihistoria, kielimu na kiitikadi

**Katika historia ya Uislamu, hakuna jina lililobeba uzito wa kielimu na mjadala mpana kama jina la Ahlu Sunnah wal-Jamaa'ah. Ni jina linalotajwa sana katika vitabu vya itikadi, mihadhara ya dini, na mijadala ya kimadhehebu. Hata hivyo, pamoja na umaarufu wake, swali muhimu limeendelea kuulizwa kwa karne nyingi: Ahlu Sunnah ni nani hasa? Je, ni jina la kila Muislamu, au ni kundi maalumu lenye sifa na vigezo maalumu? Makala hii inalenga kutoa mtazamo mmoja wa kielimu, uliokusanywa kutoka vyanzo vya wanazuoni wa Salaf (wema waliotangulia), ili kumsaidia msomaji kuelewa kwa uwazi maana ya Ahlu Sunnah, asili yake, matumizi yake, na vigezo vya kuitambulisha.**

## Maana ya neno Ahlu Sunnah

Kwa kuanza, neno Ahlu katika lugha ya Kiarabu humaanisha watu walio karibu zaidi na kitu fulani na wanaohusiana nacho kwa undani. Ndiyo maana husemwa Ahlu al-Bayt, yaani watu wa nyumbani; Ahlu al-Islam, wanaoifuata vilivyo dini ya Uislamu; na Ahlu al-Madh-hab, wanaofuata madhehebu fulani.

Kwa msingi huo, Ahlu Sunnah humaanisha watu walio karibu zaidi na Sunnah ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), wanaoishikamana nayo kwa dhati, na wanaoifuata katika nyanja zote za maisha: itikadi, ibada, na mwenendo. Sunnah hapa haimaanishi ibada peke yake, bali inajumuisha jinsi ya kumuamini Allah, jinsi ya kuelewa Qur'an, jinsi ya kuwachukulia Maswahaba, pamoja na misingi yote ya dini aliyofundisha Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

## Matumizi mawili ya jina Ahlu Sunnah

Wanazuoni wameeleza kuwa jina Ahlu Sunnah limetumika kwa maana mbili tofauti katika historia ya Uislamu.

Mosi, kwa maana ya jumla, Ahlu Sunnah humaanisha Waislamu wote wasiokuwa Raafidhwah (Shia). Katika matumizi ya kijamii na kihistoria, neno Sunni mara nyingi hutumika kama kinyume cha Raafidhwiy. Hivyo, mtu anaposema "Mimi ni Sunni," mara nyingi humaanisha "Mimi si Raafidhwiy (Shia)."

Hii ni maana ya kijamii na ya kihistoria, lakini si kipimo cha mwisho cha haki ya itikadi.

Hata baadhi ya wanazuoni wa Salaf walilitumia jina hili kwa maana hiyo, kama ilivyonukuliwa kutoka kwa Sufyan ath-Thawriy aliyesema kuwa miongoni mwa alama za Sunnah ni kuwapa kipaumbele Abu Bakr na 'Umar (radhi za Allah ziwe juu yao).

Pili, Maana ya pili ni maana ya pekee na ya kielimu, ambayo ndiyo inayokusudiwa katika vitabu vya itikadi. Kwa maana hii, Ahlu Sunnah ni wale wanaofuata Sunnah kwa usafi wake, bila kuichanganya na bidaa au matamanio ya watu.

Kwa mtazamo huu, makundi kama Khawaarij, Jahmiyyah, Murji'ah, Mashia, na makundi yote ya bidaa hayahesabiwi kuwa ni Ahlu Sunnah, hata kama yanajinasibisha na Uislamu. Sheikhul-Islam Ibn Taymiyyah anafafanua kuwa Ahlu Sunnah kwa maana hii ni Ahlul-Hadith, yaani wale wanaoegemeza itikadi yao juu ya Qur'an na Sunnah kwa ufahamu wa Maswahaba.

## Sifa za Ahlu Sunnah

Wanazuoni wakubwa wa Uislamu wamekubaliana juu ya misingi mikuu inayowatambulisha Ahlu Sunnah.

Miongoni mwa misingi hiyo ni kuthibitisha sifa za Allah kama zilivyokuja bila kuzipotosha, kuamini kuwa Qur'an ni maneno ya Allah na si kiumbe na kuamini kuwa Waumini watamuona Allah Siku ya Akhera.

Sifa nyingine ni kuamini Qadar kheri na shari yake, kuwaheshimu Maswahaba wote wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani), na kuepuka bidaa pamoja na matamanio ya kutumia akili kupita kiasi katika masuala ya dini.

Imamu Ahmad bin Hanbal, anayejulikana kama Imamu wa Ahlu Sunnah, alisisitiza kuwa yeyote anayepinga misingi hii ya Salaf hahesabiwi kuwa ni Ahlu Sunnah, hata kama anajinasibisha na jina hilo.

## Ahlu Sunnah ni akina nani kihistoria?

Kwa mtiririko wa vizazi, Ahlu Sunnah ni Maswahaba wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani), ambao ndio chimbuko la Ahlu Sunnah kwa kuwa walipokea itikadi, ibada na maelekezo ya dini moja kwa moja kutoka kwa Mtume. Kisha wakafuatiwa na Tabiina waliowafuata kwa wema na kurithi elimu ya Maswahaba kwa uaminifu.

Baada yao walikuja Ahlul-Hadith na Athar, waliolinda Sunnah, wakachambua Hadith, na kuilinda dini dhidi ya upotofu. Katika kila zama, kila anayewafuata kwa dhati, awe mwanazuoni au Muislamu wa kawaida, huhesabiwa kuwa ni miongoni mwa Ahlu Sunnah.

Naye Ibn Hazm anasema wazi kuwa hata Muislamu wa kawaida anayewafuata Salaf kwa Ikhlasi ni miongoni mwa Ahlu Sunnah.

## Mgogoro wa makundi kudai jina la Ahlu Sunnah

Kwa kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ameeleza kuwa Umma wake utagawanyika na wokovu utakuwa kwa kundi moja tu, makundi mengi yamedai kuwa wao ndio firqa najiya. Tatizo hutokea pale kundi linapojipima kwa kiongozi wake au taasisi yake, linawafanya wanaopingana nao kuwa watu wa bidaa, au linawafanya wanachama wake kuwa kipimo cha haki.

Ibn Taymiyyah anatahadharisha kuwa hali hii ni upotofu mkubwa, kwa sababu kipimo cha haki si mtu, si kundi, wala si madhehebu, bali ni Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) pekee. Kauli ya kila mtu hukubaliwa au hukataliwa, isipokuwa kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

## Kanuni ya dhahabu: haki hutangulia watu

Wanazuoni wa Salaf walisisitiza kanuni muhimu sana kwamba haki haijulikani kwa watu, bali watu hujulikana kwa haki. Hivyo, mtu haingii katika Ahlu Sunnah kwa jina analotumia, kwa kundi analojinasibisha nalo, au kwa madai anayoyatoa. Bali huingia kwa ufuasi wa kweli wa Qur'an na Sunnah kwa ufahamu wa Maswahaba, kwa kuacha bidaa, na kwa ikhlasi pamoja na unyenyekevu.

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Tanzania ijifunze kwa nchi za Kiarabu kunufaika na maji ya bahari



Tanzania ina rasilimali nyingi za maji asilia ikilinganishwa na nchi nyingi za ukanda wa Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla ikiwemo mito mikubwa inayokatiza maeneo mbalimbali ya nchi na kwa hekima ya Muumba humwaga maji yake kwenye Bahari ya Hindi, maziwa makubwa na madogo, pamoja na vyanzo vya maji ya chini ya ardhi.

Pamoja na wingi huo wa rasilimali, upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wote hauridhishi sio tu katika miji inayokua kwa kasi bali hata vijijini.

Wakati Tanzania ikipitia uhaba wa maji licha ya rasilimali nyingi ilizonazo, baadhi ya nchi zenye rasilimali chache, hususan zilizopo katika jangwa, hawana kabisa shida ya maji. HII inaonesha kuwa changamoto si uchache wa rasilimali bali mipango ya muda mrefu, usimamizi, na matumizi ya maarifa ya kisasa.

Kwa msingi huo, kuna umuhimu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kujifunza kutoka kwa uzoefu wa kimataifa ili kuondokana na dhiki hii.

## Uzoefu wa nchi za Kiarabu

Mfano wa kwanza wa kuigwa ni Saudi Arabia, nchi yenye maeneo makubwa ya jangwa na haina mito ya kudumu kama ilivyo Tanzania. Hata hivyo, Saudi Arabia imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika matumizi ya teknolojia ya kuondoa chumvi kwenye maji ya bahari (desalination) ili kuzalisha maji safi kwa matumizi ya binadamu, viwanda na kilimo.

Leo, sehemu kubwa ya maji kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika miji mikubwa ya Saudi Arabia hutokana na maji ya bahari. Uzoefu huu unaonesha kuwa mipango ya kimkakati na uwekezaji katika teknolojia vinaweza kufidia upungufu wa rasilimali hii asilia.

Falme za Kiarabu (UAE), nchi yenye fukwe ndefu za bahari lakini yenye uhaba mkubwa wa maji matamu ya asilia, ni mfano mwingine. Kupitia uwekezaji wa muda mrefu, mafunzo ya wataalamu waadilifu, na matumizi ya teknolojia za kisasa, UAE imefanikiwa kutumia maji ya bahari kuwahakikishia wananchi wake maji safi na salama kwa matumizi binafsi na hata kwa shughuli za kiuchumi.

Aidha, nchi hiyo imewekeza katika utafiti na matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza gharama za uzalishaji wa maji.

Nchi za Qatar na Kuwait nazo zinaonesha kwa vitendo umuhimu wa kulichukulia suala la maji kama jambo la kimkakati la kitaifa. Karibu maji yote ya kunywa katika nchi hizo hutokana na maji ya bahari.

Israel inatoa funzo jingine muhimu ambapo pamoja na ukame unaoikabili, imefanikiwa si tu katika (desalination) bali pia katika urejelezaji wa maji taka kwa matumizi ya kilimo, udhibiti wa upotevu wa maji, na matumizi ya teknolojia za kisasa za umwagiliaji. Leo, Israel ni miongoni mwa nchi zinazoongoza duniani katika usimamizi wa rasilimali maji na usafirishaji wa maarifa katika sekta hiyo.

## Mafunzo kwa Tanzania

Kwa kuzingatia uzoefu huo wa kimataifa, inapendekezwa Tanzania ianze kuchukua hatua za kimkakati kujifunza, hata kama kwa sasa haina uwezo wa kimizania au ulazima wa haraka wa kutumia mitambo mikubwa ya gharama kubwa ya (desalination).

Licha ya kuwa na rasilimali nyingi za maji matamu, Tanzania isichelewe kujiandaa kwa changamoto za baadaye zinazoweza kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la watu, na ukuaji wa viwanda na miji.

Hatua zinazoweza kuchukuliwa ni kupeleka wataalamu waaminifu, waadilifu na wazalendo kwenda kujifunza teknolojia na mifumo ya usimamizi wa maji katika nchi zilizoendelea katika sekta hiyo na kuimarisha programu za mafunzo na tafiti katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti kuhusu sayansi na teknolojia ya maji.

Hatua nyingine ni kuanzisha miradi midogo ya majaribio katika maeneo ya pwani ili kujifunza kwa vitendo bila gharama kubwa na pia kujifunza na kuiga sera bora za usimamizi wa maji, ikiwemo uhifadhi, urejelezaji na matumizi endelevu

Kwa ujumla, uzoefu wa Saudi Arabia, Falme za Kiarabu, Qatar, Kuwait na Israel unaonesha wazi kuwa maji ya bahari yanaweza kuwa rasilimali muhimu endapo yatatumika kwa maarifa, teknolojia na mipango ya muda mrefu. Tanzania, ambayo imejaaliwa kuwa na bahari, mito mingi na maziwa makubwa, iko katika nafasi nzuri zaidi ya kupanga mustakabali wa sekta ya maji kwa mtazamo mpana na wa kizazi hadi kizazi.

Kwa msingi huo, kujifunza kutoka kwa wenzetu si anasa, bali ni sehemu ya maandalizi ya kimkakati ya kulinda uhai, ustawi na usalama wa taifa kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

رَجَب

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803

# Mfumo wetu wa elimu una shida gani?

**Sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tuliishia na kauli kwamba shule na vyuo vyetu vimekuwa vyombo vikuu vya kueneza usekula katika jamii ya Waislamu, vikifundisha kwa ufanisi kwamba Uislamu hauna uhusiano wowote na kuuelewa ulimwengu huu, au katika kutatua matatizo yake. Leo tumalizie sehemu iliyobaki 'Insha Allah'.**

Wahitimu wengi wa vyuo na shule wamekuwa na sintofahamu na mashaka kuhusu imani yao. Hata wale Waislamu madhubuti wanaotekeleza Uislamu wao hawapewi mafunzo na kuelimishwa kuhusu namna ya kugundua na kuyapa changamoto mafundisho ya itikadi/imani za kisekula (dogmas) ambazo zimejumuishwa ndani ya mitaala yao.

Janga hili kubwa limeanza miaka ya hivi karibuni, kwa hiyo mtazamo wa kihistoria unaweza kutusaidia. Kwa karne nyingi, jamii zetu, utamaduni, na mfumo wa elimu vilikuwa huru na utenganisho wa usekula na dini. Shule zetu zilifundisha masomo yote muhimu kwa kutumia mbinu asilia isiyotenganisha dini na dunia.

Kwa kuwa Waislamu walikuwa viongozi katika fani zote za sayansi (mpaka karne ya 15 miladia), masomo kama kemia, tiba (medicine) na unajimu (astronomy) hayakuwa na utenganisho wa kisekula.

Utenganisho ulianza katika ulimwengu wa Magharibi wakati wa zama zake za mwamko (Renaissance) ambapo ulitupilia mbali imani za kibubusa, ambazo zilikuwa ni mzigo, na walipata njia ya haraka ya maendeleo ya vitu kwa kutumia mbinu za kisekula. Mapinduzi ya viwanda yaliwapa kasi zaidi, ukoloni ukaleta itikadi ya kisekula na dini ya usekula katika ardhi za Waislamu.

Katika zama hizi, Waislamu walikuwa dhaifu katika maeneo kadhaa, wakasalimisha uongozi wao katika elimu na maarifa (Intellectual leadership) kwa nchi za Magharibi, na wakawa wameshindwa kuendana na kasi ya maendeleo ya kisayansi, hatimae wakajikuta katika hali ngumu.

Iwapo wangekubali na kufundisha watoto wao sayansi za Kimagharibi, basi pia wangekuwa wanawafundisha 'dogmas' za kupinga Uislamu. Na iwapo wangejitenga na kukaa peke yao, wangeachwa nyuma katika maendeleo ya sayansi na vitu.

Katika kujibu changamoto hiyo, Waislamu walitumia njia mbili. Kwanza, taasisi zetu za elimu (Daarul – Uloom) zilihifadhi maarifa na maadili ya Kiislamu kwa kuyafungia kabisa dhidi ya athari za Kimagharibi. Ni kutokana na jitihada hizo ndiyo maana maarifa ya Kiislamu yako vizuri mpaka leo.

**Hebu tuulize, katika ulimwengu mpana wa Waislamu, kuna shule yoyote ya Kiislamu inayofundisha sayansi, ambapo wahitimu wake wanaweza kuipa changamoto nadharia ya 'Evolution' ya Darwin kwa misingi ya kisayansi?**


Na kule ambako jambo hili walilizembea, kama ilivyo katika baadhi ya nchi za Waislamu, matokeo yake yalikuwa ni kuchakachua (compromise) msimamo wao wa Kiislamu bila faida yoyote katika ubora wa elimu. Lakini pia, hawana uwezo wa kutoa uongozi katika maeneo mengi ya jamii.

Jukumu hilo limekwenda kwa wahitimu wa shule na vyuo vya mtindo wa Kimagharibi. Isivyo bahati, shule hizo na mitaala yake inapalilia njia za kisekula za kuutazama ulimwengu huu na kutatua matatizo yake. Mivutano iliyoanzishwa na mifumo hii miwili inayopingana ya elimu, inaweza kuonekana leo katika kila nchi ya Waislamu. Utenganisho huu wa elimu lazima ukome.

Waislamu hatuwezi kusonga mbele bila ya kurekebisha elimu yetu, na hatuwezi kusimamisha Uislamu kwa ukamilifu katika jamii zetu bila kuzalisha raia walioelimika na viongozi wanaohitajika kwa jamii ya Kiislamu. Huu ndiyo wakati wa kuunda mitaala jumuishi ya Kiislamu na kuondoa upotofu wa kisekula kwenye elimu yetu yote.

Kujenga shule nyingi zaidi na vyuo ni jambo jema, lakini siyo jibu pekee. Kuendeleza taasisi za kielimu zinazoweza kufundisha kila somo kwa muktadha mzuri wa Kiislamu ndiyo jibu hasa. Ni kazi kubwa! Lakini bila hivyo tutaendelea kueneza ujinga kwa jina la elimu.

***Itaendelea wiki ijayo Insha Allah***






# Mali fedha za Kiislamu kufikia dola trilioni 6 mwaka huu

Sekta ya fedha za Kiislamu duniani inatarajiwa kuvuka kiwango cha dola trilioni 6 za mali ifikapo mwisho wa mwaka 2026, kutokana na ukuaji mkubwa unaochochewa na benki za Kiislamu, masoko ya mitaji, sukuk na teknolojia ya kifedha (fintech) inayokua kwa kasi barani Asia, nchi za Ghuba na Afrika.

Kwa mujibu wa AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics, jumla ya mali za fedha za Kiislamu zilifikia dola trilioni 5.2 mwaka 2025, ongezeko la asilimia 14.9 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Akizungumza kuhusu mwelekeo huo, Mtendaji Mkuu wa kituo hicho, Zubair Mughal, alisema sekta hiyo sasa imekuwa sehemu muhimu ya mfumo wa fedha wa kimataifa licha ya changamoto za mfumuko wa bei, hatari za kisiasa na masharti magumu ya kifedha.

Benki za Kiislamu zinaendelea kuongoza sekta hiyo kwa kuchangia asilimia 72 ya mali zote, huku ufadhili ukiongezeka kwa zaidi ya asilimia 17 na amana kukua kwa karibu asilimia 9 mwaka 2025. Ukuaji mkubwa umeonekana katika nchi za Ghuba (GCC), Asia na masoko kadhaa ya Afrika, ambapo baadhi ya nchi ziliripoti ongezeko la zaidi ya asilimia 20.

Soko la sukuk pia lilifanya vizuri, likirekodi utoaji wa zaidi ya dola bilioni 230 mwaka 2025, huku nchi kama Tanzania, Zambia na Kenya zikichangia kuunganisha Afrika na masoko ya kimataifa ya sukuk.

Aidha, fintech ya Kiislamu imeibuka kuwa eneo linalokua kwa kasi zaidi, ikichochewa na huduma za malipo ya kidijitali, mikopo inayozingatia Shariah na matumizi ya akili bandia.

Kwa mtazamo wa baadaye, wataalamu wanaona Afrika kama eneo lenye fursa kubwa zaidi ya ukuaji, huku wakisisitiza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuhakikisha uthabiti wa muda mrefu wa sekta hiyo.








# Russia yajaribu benki za Kiislamu majimbo yenye Waislamu wengi



Russia imeanzisha rasmi mfumo wa majaribio wa benki za Kiislamu katika majimbo manne yenye Waislamu wengi—Tatarstan, Bashkortostan, Chechnya na Dagestan—ikiwa ni hatua muhimu ya kupanua ujumuishaji wa kifedha kwa jamii yake ya Kiislamu inayokua.

Mpango huu unalenga kutoa huduma za kifedha zinazozingatia misingi ya Shariah, ikiwemo kuepuka riba na kuhimiza biashara halisi na ushirikishwaji wa hatari.

Hatua hiyo inaifanya Russia ijiunge na nchi ambako benki za Kiislamu zimekomaa, kama Pakistan, Saudi Arabia, Malaysia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Indonesia na Qatar, ambako fedha zinazozingatia Shariah zinatumika kama mbadala kamili wa benki za kawaida.

Wachambuzi wa masuala ya fedha wanasema mpango huu umeanza kuvutia macho ya masoko ya kimataifa, huku taasisi za kitaaluma na wataalamu kutoka Uingereza, Marekani, Kanada na Ufaransa wakiutazama kama mfano unaotekelezeka wa fedha zenye maadili katika nchi zisizo na Waislamu wengi.

Iwapo jaribio hili litafanikiwa, linatarajiwa kuimarisha uhusiano wa kiuchumi wa Russia na ulimwengu wa Kiislamu, sambamba na kuipa nchi hiyo njia mbadala ya kuboresha na kuupanua mfumo wake wa fedha.

Anatoly Aksakov, mwenyekiti wa Kamati ya Masoko ya Fedha ya Bunge la Russia (State Duma) na pia mwenyekiti wa Baraza la Chama cha Benki za Russia, akizungumza katika kituo cha mjini Kazan cha Shirika la Kimataifa la Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI) amesema mpango huo mpango huo uliandaliwa kwa kushirikiana na wafanyabiashara, hususan wanaowakilisha jamii ya Kiislamu nchini Russia.

Russia ina takribani Waislamu milioni 20, sawa na asilimia 14 hadi 15 ya idadi ya watu, hali inayofanya fedha za Kiislamu kuwa na umuhimu mkubwa katika mustakabali wa mfumo wa fedha wa nchi hiyo.

Hatua ya kuanzishwa kwa benki ya Kiislamu inatazamwa kama fursa ya kuimarisha ujumuishaji wa kifedha, kukuza biashara na kuleta mbadala wa maadili katika sekta ya benki ya Russia.

## AlHuda yaitaja Tanzania vizuri soko la Sukuk Afrika

**Tanzania imetajwa miongoni mwa nchi mpya za Afrika zilizoingia kwa nguvu kwenye soko la kimataifa la sukuk, hatua inayochukuliwa kuwa muhimu katika kuimarisha sekta ya fedha za Kiislamu na kuvutia mitaji ya maendeleo inayozingatia misingi ya Shariah.**

**Kwa mujibu wa tathmini ya shirika la AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics, Tanzania sambamba na Zambia na Kenya zimechangia kwa kiasi kikubwa kuiunganisha Afrika na masoko ya kimataifa ya sukuk, hususan kupitia mahitaji ya ufadhili wa miradi ya miundombinu na maendeleo ya taifa.**

**Soko la sukuk lilionekana kufanya vizuri mwaka 2025, likirekodi utoaji wa zaidi ya dola bilioni 230 duniani kote.**

**Wataalamu wa masuala ya fedha wanasema ushiriki wa Tanzania katika soko hilo ni fursa ya kupanua vyanzo vya fedha, kupunguza utegemezi wa mikopo yenye riba, na kuvutia wawekezaji wanaotafuta bidhaa za kifedha zenye maadili.**

**Hatua hiyo pia inaashiria kuongezeka kwa nafasi ya Tanzania katika mfumo wa fedha za Kiislamu unaokua kwa kasi barani Afrika. Wachambuzi wanaeleza kuwa iwapo mifumo ya kisheria na udhibiti itaendelea kuimarishwa, Tanzania inaweza kuwa kitovu muhimu cha sukuk katika Afrika Mashariki.**

فتاوى رَجَب



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

# Ni nani Ahlu Sunnah wal-Jamaa'h?

***Jibu:*** Ahlu Sunnah wal-Jamaa'h ni wale Waislamu wanaoshikamana na mafundisho ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na kuyaishi. Wameitwa "Watu wa Sunna" kwa sababu wameishikilia Sunna. Wameitwa "Watu wa Jamaa'h" kwa sababu wamekusanyika pamoja kwenye mafundisho yake bila kugawanyika.

Wale wanaoanzisha mambo mapya yasiyo ya dini (bid'a) wanatofautiana na hawafuati Sunna, jambo linaloonesha wanaacha njia sahihi ya dini. Kwa ufupi, Ahlu Sunna wal-Jamaa'a ni sawa na kusema Waislamu wanaofuata Sunna na kuiishi bila kuongeza bidaa.

Na Allah Ndiye Mjuzi zaidi

***Swali:* Wakati wa kumuingiza maiti mwanamke kaburini, baadhi ya watu hufunika shuka (au kitambaa) juu ya kaburi, na wakati mwingine haingii kaburini kupokea maiti isipokuwa mahramu wake tu. Je, hilo lina hukumu gani?**

***Jibu:*** Ama kuhusu kufunika shuka juu ya kaburi wakati wa kumshusha maiti mwanamke, jambo hilo ni zuri, kwa maana, linaruhusiwa na linapendekezwa. Wanazuoni wametaja hilo na wakasema kuwa kaburi la mwanamke hufunikwa wakati wa kumuingiza kwenye mwanandani wake, yaani hufunikwa kwa ajili ya sitara (heshima na faragha).

Ama kuhusu watu wa kuingia kaburini, si lazima awe mahramu wake pekee. Inajuzu (inaruhusiwa) kumuingiza maiti kaburini mahramu wake (ndugu wa karibu) au mtu mwingine asiye mahramu.

Dalili ya jambo hilo ni pale Mtume (Allah amshushie rehema na amani) katika mazishi ya mmoja wa binti zake, aliposema: "Ni nani kati yenu ambaye hakufanya jimai usiku uliopita?"

Abu Twalha akasema: "Mimi." Mtume wa Allah, (Allah amshushie rehema na amani) akasema: "Shuka (uingie kaburini)."

Basi, Abu Twalha akashuka na kumuingiza maiti kaburini, hali ya kuwa mume wake (Uthman Allah amridhie) alikuwepo, na baba yake, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), pia alikuwepo.

Na Allah Ndiye Mjuzi zaidi

***Swali:* Ni kweli kwamba kumuenzi na kumheshimu mtu aliyekufa ni kumzika haraka? Na ni wakati gani si vyema kumzika mtu aliyekufa?**

***Jibu:*** Hukumu ni kwamba ni sunna kumzika maiti haraka baada ya kufa, hivyo ni kweli kuwa kumzika mtu haraka ni kumuenzi na kumheshimu maiti. Hii inajulikana hivyo katika dini yetu.

Kwa hiyo, maana ya hadith inayohusishwa na Ali (Allah amridhie) kwenye hili inayohimiza kumzika mtu haraka baada ya kufa, ni sahihi na hivyo kufanya hivyo ni sunna.

Hata kama maneno haya hayajathibitishwa moja kwa moja kutoka kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), Imam Ahmad aliyaripoti kutoka kwa Ali (Allah amridhie) kwamba: "Kuna mambo matatu usiyachelewe, unapoingia wakati wa kusali, mazishi, na mjane anapopata mwenza anayekidhi vigezo na masharti (ndoa)."

Ama kuhusu muda, kuna nyakati tatu ambazo si vyema kuzika mtu, mosi wakati Jua linapochomoza mpaka lipande juu; pili, wakati jua lipo katikati ya mchana; na tatu, wakati jua linapokaribia machweo. Katika nyakati hizi, siyo sahihi kusali au kuzika wafu.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

***Swali:* Kuna mtu anataka kutoa zaka ya mali yake kwa jamaa anayestahiki lakini jamaa anajulikana kutokuwa na matumizi mazuri ya fedha, yaani kwa mfano, pesa ya kutosha mwezi mzima, ataitumia ndani ya wiki moja. Je, mtoa zaka anaweza kushikilia pesa hizo kwa miezi kadhaa kwa lengo kumpa kidogo kidogo kulingana na mahitaji yake kila mwezi?**

***Jibu:*** Ikiwa mtu anayetoa zaka ana mamlaka au jukumu la kumhudumia huyo jamaa (kama mlezi au muwakilishi), hakuna tatizo kushikilia pesa hiyo na kumpelekea kidogo kidogo.

Vinginevyo, ikiwa hana mamlaka juu yake, anapaswa kumpa kiasi cha muda mfupi kinachokidhi mahitaji yake, na baki ya pesa iweze kugawanywa kwa wanyonge wengine ambao wanaostahiki zaka.

Na Allah Ndiye Mjuzi zaidi

MAHMOUD NYAMGUMA

# Licha ya mapatano, Israel yazidi zuia misaada Gaza



Baraza la Mahusiano ya Kiislamu la Marekani (Council on American-Islamic Relations – CAIR) limelaani uamuzi wa Israel kusimamisha mashirika ya misaada ya kibinadamu yanayofanya kazi Gaza, likisema ni ukiukwaji wa wazi wa sheria za kimataifa na shambulio dhidi ya utu wa binadamu, wakati raia wa Kipalestina wakikabiliwa na janga kubwa la kibinadamu.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao wa X, CAIR ilisema kupigwa marufuku kwa Doctors Without Borders (Médecins Sans Frontières) pamoja na mashirika mengine 36 ni "kitendo cha kikatili kisicho na mfano."

CAIR wamesisitiza kuwa wahudumu wa misaada si wapiganaji na kwamba msaada wa kuokoa maisha haupaswi kutumiwa kama silaha ya vita. CAIR pia imelihimiza Bunge la Marekani kuchukua hatua za haraka kulinda wahudumu wa kibinadamu na kuhakikisha misaada inaingia Gaza bila vikwazo.

Kwa mujibu wa CAIR, kulengwa kwa mashirika ya misaada ni ukiukwaji wa sheria za kibinadamu za kimataifa, msimamo unaoungwa mkono na UN Office for the Coordination of Humanitarian Affairs (OCHA), ambayo imeonya mara kadhaa kuwa vizuizi vya misaada vinaongeza vifo vinavyoweza kuzuilika, hasa kwa watoto, wanawake na wazee.

Israel imetetea uamuzi wake ikidai mashirika hayo hayakukidhi masharti mapya ya usajili na uhakiki.

Doctors Without Borders imeonya kuwa masharti hayo yanaweza kuwaacha mamia ya maelfu bila huduma muhimu za afya mwaka 2026, na kuzidisha mgogoro uliopo.

Licha ya makubaliano ya kusitisha mapigano kuanza Oktoba, Israel bado inazuia misaada muhimu kuingia Gaza, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) likisema zaidi ya asilimia 60 ya vituo vya afya Gaza havifanyi kazi kikamilifu kutokana na uhaba wa dawa na vifaa.

Maafisa wa Palestina wanasema watu 414 wameuawa Gaza tangu kusitishwa kwa mapigano, jambo linaloongeza shinikizo kwa jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua. CAIR imesisitiza kuwa ukimya wa kisiasa, hususan kutoka Washington, umeiwezesha Israel kuendelea na kile inachokiita mauaji ya kimbari yanayofadhiliwa na walipa kodi wa Marekani.

Chanzo: Anadolu Ajensi

## Ripoti: Waislamu Uingereza wakarimu mara nne zaidi

**Ripoti mpya imebainisha kuwa Waislamu wa Uingereza ni miongoni mwa wachangiaji wakubwa zaidi wa misaada ya kijamii nchini humo, wakitoa takribani pauni bilioni 2.2 kila mwaka, kiasi ambacho ni karibu mara nne ya wastani wa mchango wa mtu mzima nchini Uingereza.**

**Ripoti hiyo yenye kichwa Building Britain: British Muslims Giving Back imeandaliwa na Equi, ikichambua mchango wa Waislamu wa Uingereza katika misaada ya ndani na ya kimataifa.**

**Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ukarimu huo unatokana kwa kiasi kikubwa na mafundisho ya Kiislamu, hususan Zaka, sadaka ya lazima ya asilimia 2.5 ya mali ya ziada, na Sadaka, ambayo ni utoaji wa hiari. Zaka pekee inakadiriwa kuchangia hadi asilimia 40 ya fedha zote zinazokusanywa na taasisi za misaada za Kiislamu. Tafiti za maoni zilizofanywa na Savanta zinaonyesha kuwa nusu ya wachangiaji Waislamu wanapanga kuongeza michango yao.**

**Ingawa sehemu kubwa ya misaada imekuwa ikienda kwenye shughuli za kibinadamu nje ya nchi, ripoti inaonyesha mwelekeo mpya wa kizazi cha vijana wa Kiislamu kuunga mkono miradi ya ndani, ikiwemo kupambana na umaskini, ukosefu wa makazi na matatizo ya afya ya akili. Taasisi kama National Zakat Foundation, Islamic Relief UK na Al-Khair Foundation zimetajwa kwa mchango wao mkubwa nchini humo.**

MAHMOUD NYAMGUMA




# Dunia yachukizwa jaribio la ukoloni la Marekani nchini Venezuela

Hatua ya Marekani kufanya mashambulizi ya kijeshi nchini Venezuela na kumkamata Rais wa nchi hiyo, Nicolás Maduro, imezua mshtuko na kulaaniwa vikali na mataifa mengi duniani, huku ikitafsiriwa kama jaribio jipya la ukoloni na ukiukwaji mkubwa wa sheria za kimataifa.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alisema mashambulizi hayo yalikuwa ya "kiwango kikubwa" na kwamba Maduro pamoja na mkewe wamepelekwa nje ya nchi hiyo na sasa wako chini ya ulinzi wa Marekani.

Serikali ya Venezuela imezitaja hatua hizo kama "uchokozi mkubwa wa kijeshi" na kuvishutumu vikosi vya Marekani kwa kushambulia ardhi na raia wa Venezuela bila uhalali wa kisheria.

Mashambulizi hayo yaliripotiwa kufanyika alfajiri, yakisababisha hofu kubwa jijini Caracas ambako milipuko na ndege za kivita ziliripotiwa kusikika.

Nchi kadhaa za Amerika ya Kusini, Ulaya, Asia na Mashariki ya Kati zimelaani vikali hatua ya Marekani. Rais wa Colombia, Gustavo Petro, alisema shambulio hilo ni ukiukwaji wa mamlaka ya Venezuela na tishio kwa amani ya eneo la Amerika ya Kusini.

Cuba, Mexico na Brazil zimesisitiza kuwa matumizi ya nguvu dhidi ya taifa huru yanakiuka Mkataba wa Umoja wa Mataifa na yanafungua mlango wa machafuko makubwa ya kimataifa.

China na Urusi pia zimelaani vikali shambulio hilo, zikisema ni mfano wa tabia za kihegemoni za Marekani na tishio kwa amani ya dunia. Beijing ilisema inasikitishwa sana na matumizi ya nguvu dhidi ya taifa huru, huku Moscow ikionya kuwa kitendo hicho kinaweza kusababisha mgogoro mpana wa kikanda.

Iran nayo ilisisitiza kuwa mataifa yanapaswa kusimama kidete kupinga mashinikizo ya kigeni yanayovunja uhuru wa nchi nyingine.

Katika Umoja wa Ulaya, Ufaransa, Uhispania, Ujerumani na Italia zimetaka tahadhari, mazungumzo na kuheshimiwa kwa sheria za kimataifa.

Ufaransa ilisema kukamatwa kwa kiongozi wa taifa kwa nguvu za kijeshi ni kinyume cha misingi ya uhusiano wa kimataifa, huku Uhispania ikijitolea kusaidia juhudi za upatanishi. Umoja wa Ulaya kwa ujumla umetaka pande zote zijizuie na kulinda usalama wa raia.

Licha ya baadhi ya viongozi wachache, kama Rais wa Argentina, kupongeza hatua

Na Wwandishi wetu




# Australia wakaa misikitini kulinda usalama wao

Jamii ya Waislamu nchini Australia imeanza kuchukua hatua za kujilinda kwa kukesha na kulala misikitini usiku, kufuatia ongezeko la vitendo vya chuki na Uislamofobia baada ya shambulio la Bondi lililotokea Desemba 14.

Hatua hiyo imeshuhudiwa katika majimbo ya New South Wales, Victoria na Queensland, huku misikiti kadhaa zikikumbwa na vitisho, uharibifu wa mali na matusi yanayolenga Uislamu.

Kwa mujibu wa Australian National Imams Council (ANIC) matukio ya chuki dhidi ya Waislamu yameongezeka kwa karibu asilimia 200 tangu tukio hilo. Takwimu zinaonesha kuwa angalau misikiti na vituo vya Kiislamu tisa vimeripoti uharibifu au vitisho vikubwa vilivyohitaji kuingilia kati kwa polisi.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la matukio kutoka wastani wa 1–2 kwa siku hadi takribani 18 kwa siku, yakihusisha matusi, uharibifu wa mali na mashambulizi ya maneno mtandaoni.

Katika eneo la Minto Mosque kusini-magharibi mwa Sydney, wanajamii wameanza kukesha usiku kucha kulinda msikiti dhidi ya hujuma. Kamati ya msikiti imesema hofu imeenea, hasa kwa wanawake wanaovaa hijab ambao wamekuwa walengwa wakuu wa matusi na vitisho.

Hali kama hiyo imeripotiwa Melbourne, ambako Msikiti wa Waalbania ulioko Carlton ulipokea barua pepe ya chuki kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, ikiwataka Waislamu "kuondoka" nchini Australia.

Viongozi wa Kiislamu wamesema kinachotia wasiwasi zaidi ni kuhusishwa kwa Uislamu na ugaidi, licha ya mashirika ya Kiislamu kulaani vikali shambulio la Bondi. ANIC imesisitiza kuwa itikadi na matendo ya makundi ya kigaidi kama ISIS/Daesh hayana uhusiano wowote na mafundisho ya Uislamu, wakisisitiza, vitendo vya mtu mmoja haviwezi kuwakilisha dini au jamii nzima.

Takwimu zinaonesha athari za moja kwa moja kwa maisha ya kila siku ya Waislamu. Islamic Council of Victoria (ICV) imeripoti kupokea makumi ya simu za vitisho na kulazimika kufunga maoni kwenye mitandao ya kijamii kutokana na lugha ya chuki. Wataalamu wa haki za binadamu wanasema hali hii ni adhabu ya pamoja kwa jamii ya Waislamu na inakiuka misingi ya haki, usawa na uhuru wa kuabudu.

Viongozi wa jamii sasa wanaitaka serikali kuchukua hatua za kisheria na kuelimisha jamii dhidi ya chuki ya uislamofobia, kama inavyopambana na chuki dhidi ya Wayahudi.

Wanaharakati wa Kiislamu wanasema kulinda usalama wa Waislamu ni kipimo cha dhamira ya Australia katika kulinda haki, mshikamano na utu wa kila raia bila kujali dini au asili.

Chanzo: Australian Broadcasting Corporation




NASAHA
ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Nini ufanye, uache katika mwezi wa Rajab

**Tumo katika mwezi wa Rajab, ambao kwa mujibu wa Kalenda ya Kiislamu (Al–Hijri) ni miongoni mwa miezi minne Mitakatifu aliyotujulisha Mwenyezi Mungu ndani ya Qur' an: "Hakika idadi ya miezi mbele ya Allah ni miezi kumi na miwili tangu siku aliyoumba mbingu na ardhi; katika hiyo, minne ni mitakatifu, hiyo ndiyo dini ya sawa kwa hiyo msizidhulumu nafsi zenu ndani**

Miezi Mitakatifu iliyokusudiwa ndani ya Aya hii ni Dhul–Qa'ada (Mfunguo pili), Dhul–Hijja (Mfunguo tatu), Muharram (Mfunguo nne) na mwezi huu wa Rajab. Wanazuoni wa fani ya historia (Tareikh) wamesema kuwa, mwezi huu Mtakatifu umeitwa Rajab Mudhwarra kutokana na kutamalaki utulivu ndani yake kwa watu kuweka silaha chini pindi unapoingia.

Yaani hata kama kuna vita vinaendelea ndani ya mwezi huu vinapaswa kusimama isipokuwa vita vya kuinusuru dini. Kwa miaka mingi, hili lilikuwa likifanyika hata kabla ya mafundisho aliyokuja nayo Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani iwe juu yake).

Allah ameweka msisitizo zaidi kuhusu kuiheshimu miezi yote minne Mitakatifu kwa kusema: "Enyi mliyoamini, msivunje utukufu wa alama za Allah wala miezi Mitakatifu..." [Qur' an, 5:2].

Kwa hiyo, kinachotakikana katika mwezi huu wa Rajab na miezi mingine Mitakatifu ni Waislamu kumcha Allah Ta'ala kwa kuepuka makatazo yote ikiwa ni pamoja na matendo na imani potofu. Hata hivyo, inasikitisha kuona tulio wengi hatuupi umuhimu mwezi huu wa Rajab kama ilivyo kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, pamoja na faida lukuki zinazopatikana ndani yake.

Kwa hali hii, si ajabu wapo miongoni mwetu Waislamu ambao hawafahamu umuhimu na fadhila za mwezi wa Rajab. Hivyo basi, ipo haja kwa viongozi wa dini hususan Maimam wa misikiti kuelezea faida zinazopatikana katika mwezi huu sanjari na kuwahimiza Waumini wao kufanya mambo ya kheri.

Zipo amali nyingi njema ambazo Muislamu anaweza kuzifanya, lakini jambo la msingi ni mtu kujilazimisha kufanya heri kadiri awezavyo. Allah anatuambia: "Basi Mcheni Mwenyezi Mungu kadiri muwezavyo (mwisho wa jitihada yenu), na sikieni, na tiini, na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndiyo waliofanikiwa." [Qur'an, 64:16].

Ni muhimu kuelewa kuwa kila neema aliyoruzukiwa mja na Allah Ta'ala itaulizwa siku ya Kiyama. Hivyo, ndugu yangu katika imani, tumia vyema fursa ya afya na uzima katika kumuabudu Allah Ta'ala kadiri itakavyowezekana kwani kufanya amali njema katika mwezi huu kuna ujira mkubwa.

Haipasi Muislamu kumuasi Allah Ta'ala ndani ya mwezi wa Rajab kwani kutenda maovu katika mwezi huu madhambi yake huwa ni makubwa zaidi na ndiyo maana Allah ametuambia: "Basi mzidhulumu nafsi zenu humo." [Qur' an, 9:36].

Katika ufafanuzi wake kuhusu Aya hii, Imam Qatada (Allah amrehemu) amesema: "Dhuluma itakayotendeka katika miezi Mitakatifu ni mbaya na kubwa zaidi kuliko dhuluma itakayotendeka katika miezi mingine. Hakika dhuluma daima ni makosa, lakini Allah hufanya baadhi ya vitu kuwa vizito kuliko vingine..." [Tafsiri ya Qur'an–Ibn Kathir].

Kwa maelezo hayo, hatuna budi kujipinda kufanya ibada mbalimbali ndani ya mwezi huu sanjari na kujiepusha na kufanya madhambi.

## Yaliyokatazwa katika mwezi wa Rajab

Miongoni mwa mambo tuliyokatazwa kufanya katika mwezi huu ni kupigana vita. Allah Mtukufu anasema: "...kupigana vita wakati huo (wa miezi mitakatifu) ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasiende katika njia ya Allah na kumkanusha yeye (Allah), na kuzuilia watu wasiende kwenye msikiti Mtukufu (Makka), na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Allah. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuua...." [Qur'an, 2:217].

Kadhalika, imeharamishwa katika mwezi wa Rajab kumshirikisha Allah kwa aina zote za shirk, kuiba, kuzini, kucheza kamari, kunywa pombe, kudhulumiana, kugombana, kutukanana, kuvunjiana heshima, kusema uongo, kuwaasi wazazi wawili, kusengenya na kadhalika.

Kwa baadhi ya Waislamu imekuwa kawaida kwao kufanya mambo ya kizushi (bid'a) ndani ya mwezi huu, ikiwamo kufanya dua na dhikri mbalimbali ambazo hazijathibiti kufanywa na Mtume wala Masahaba, na wengine wameufanya mwezi huu kuwa mahsusi wa kuzuru makaburi, jambo ambalo linapaswa kufanywa wakati wowote ule kama alivyoamuru Mtume wa Allah.

Mara nyingi tukiyasema haya tunaambiwa tunaleta mambo mapya. Mwanazuoni Al–hafidh Ibn Hajar Al–Asqalani (Allah amrehemu) amesema: "Hakuna hadith sahihi inayoweza kutumika kama ushahidi wa kuonesha fadhila za (mwezi) Rajab au kufunga swaumu ndani yake au kusimama usiku." [Taz: 'Tabayyun al–Ajab bimaa warada fii Fadhli Rajab']. Hivyo tujiepushe kufanya mambo ambayo hayana faida na sisi tukiamini kuwa tunajikurubisha kwa Allah.

## Yapi ya kufanya

Hakuna shaka kwamba kutenda heri ndani ya mwezi huu malipo (thawabu) yake huwa ni makubwa zaidi.

Kwa kuzingatia ukweli huo, sisi Waislamu hatuna budi kutumia fursa hiyo kufanya mambo ya kheri ikiwamo kumuomba Allah msamaha na kutubia madhambi, kumtaja Allah kwa wingi, kusoma Qur'an, kufunga swaumu za sunna, kutoa sadaka, kusaidia yatima, wajane na masikini, kuwatendea wema wazazi wawili, majirani na marafiki, kuamrishana mema na kukatazana maovu, kupatanisha waliogombana, na kadhalika.

Ni muhimu tutumie siku za mwezi wa Rajab kufanya ibada mbalimbali za wajibu na Sunna sambamba na kuacha yaliyoharamishwa kwa kuzingatia maonyo ya Allah Aliyetukuka: "Enyi mliyoamini, msivunje utukufu wa alama za Allah wala miezi Mitakatifu..." [Qur' an, 5:2].

JUNAYNAT ALLY DAMA




# Ratiba ya asubuhi inavyoathiri ufanisi siku nzima

Utafiti wa kisayansi unaendelea kuthibitisha jambo ambalo watu wengi hulihisi kwa uzoefu wa maisha ya kila siku: jinsi unavyoanza siku yako huamua kwa kiasi kikubwa namna utakavyofanya kazi kiakili, kihisia na hata kimwili siku nzima.

Asubuhi si mwanzo wa siku tu, bali ni hatua ya mpito muhimu inayouandaa ubongo kutoka katika hali ya mapumziko kwenda kwenye hali ya utendaji.

Makala ya kisayansi iliyoandikwa na Vijay Kumar Malesu na kuchapishwa na tovuti ya News Medical inaeleza kuwa ratiba ya asubuhi inayolingana na saa ya mwili (circadian rhythm) husaidia kuboresha uwezo wa kufikiri, kudhibiti hisia na kuimarisha ubora wa usingizi.

Saa ya mwili ni mfumo wa kibaolojia unaodhibiti usingizi, homoni, joto la mwili na kiwango cha umakini. Ratiba ya asubuhi inapolingana na saa hii ya asili, ubongo hufanya kazi kwa ufanisi zaidi na mwili hujiandaa vyema kukabiliana na mahitaji ya siku.

Kwa mujibu wa tafiti hizi, ratiba bora ya asubuhi hujumuisha vipengele vinavyofanya kazi kwa pamoja kama mfumo mmoja: mwanga wa asubuhi, kuamka kwa muda uleule kila siku, unywaji wa maji, harakati za mwili, lishe sahihi na mazoea ya kutuliza akili kama kutafakari au kupumua kwa utaratibu.

## Mwanga wa asubuhi

Mwanga wa asubuhi una nafasi ya kipekee katika kuamsha mfumo wa fahamu. Ndani ya ubongo kuna sehemu iitwayo suprachiasmatic nucleus (SCN) ambayo hupokea taarifa za mwanga kutoka machoni. Taarifa hizi hupunguza uzalishaji wa homoni ya melatonini inayosababisha usingizi na kuupa mwili ishara kuwa ni wakati wa kuwa macho na makini.

Utafiti unaonyesha kuwa kujianika kwenye mwanga wa asili mapema asubuhi husaidia kusawazisha mzunguko wa usingizi na kuamka, kuongeza umakini wa akili na hata kuboresha hali ya hisia. Hata katika mazingira magumu kama ya baridi kali ya Antarctica, mwanga mkali wa asubuhi uliweza kuboresha uwezo wa kufikiri na kusawazisha saa ya mwili.

## Kuamka muda uleule

Kuamka muda uleule kila siku ni nguzo muhimu ya ratiba bora ya asubuhi. Uthabiti huu huisaidia saa ya mwili kufanya kazi kwa mpangilio, hivyo kuboresha usingizi wa usiku na umakini wa mchana.

Tafiti zinaonyesha kuwa kubadilisha mara kwa mara ratiba ya usingizi kunahusishwa na msongo wa mawazo, hisia za huzuni na afya duni ya akili. Kuamka kuchelewa au kubaki kitandani kwa muda mrefu huongeza hali ijulikanayo kama sleep inertia, ambayo hupunguza kasi ya akili na huchelewesha kuanza kwa siku kwa ufanisi.

## Maji na lishe

Baada ya saa kadhaa za usingizi, mwili huwa katika hali ya upungufu wa maji. Kunywa glasi ya maji mara tu baada ya kuamka husaidia kuamsha kimetaboliki na kuboresha kazi za ubongo. Upungufu mdogo tu wa maji umehusishwa na kupungua kwa umakini, kumbukumbu na uthabiti wa hisia.

Vivyo hivyo, kifungua kinywa chenye uwiano mzuri huchangia kati ya asilimia 20 hadi 35 ya nishati ya siku nzima. Tafiti zinaonyesha kuwa watu wanaokula kifungua kinywa mara kwa mara hupata virutubisho muhimu zaidi kama protini, nyuzinyuzi na madini, hali inayosaidia kudhibiti hisia na kuimarisha umakini wa akili kwa muda mrefu.

## Mazoezi

Mazoezi mepesi au ya wastani ya asubuhi huchochea mzunguko wa damu na kuongeza hewa ya oksijeni kwenye ubongo. Hii huongeza umakini na hisia chanya kwa saa kadhaa. Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa mazoezi ya asubuhi yanaweza kuboresha hali ya hisia na uwezo wa kuzingatia kazi hadi masaa 12 baadaye.

Sambamba na hilo, mazoea ya kutuliza akili kama kutafakari (meditation), kupumua kwa kina pia husaidia kupunguza homoni ya msongo wa mawazo (cortisol).

## Muhimu zaidi: Sala (Swalatul-Fajr)

Swala hii huashiria kuanza kwa siku kwa kumkumbuka Allah, na hivyo humpa Muumini ulinzi wa Mwenyezi Mungu, utulivu wa ndani na mwanga wa kiroho, hivyo kuweka mwelekeo mwema wa matendo yote ya siku nzima. Sala hii pia hutoa utulivu wa kiroho na kisaikolojia unaoiweka akili katika hali ya unyenyekevu, umakini na nidhamu kabla ya kuanza shughuli za siku.


Radio
Imaan FM
Arusha
90.8fm
Mwanza
106.5fm
Mbeya
90.3fm
Tabora
101.6fm
Ruvuma
94.2fm
Mtwara
90.9fm
Kigoma
92.5fm
Sikiliza
104.5FM
Dar es Salaam
Elimu Bila Mipaka




MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Tuige nidhamu, uchapaji kazi wa Mitume

Abdulrahman bin Auf (Allah amridhie) ni mfano wa juu kabisa katika kumtegemea Allah (tawakkul), kuchukua sababu, kujisitiri (kujilinda na kuomba) na kutafuta kipato halali. Hii ni simulizi nzuri, yenye mvuto na uwazi mkubwa, inayotufafanulia kauli ya Allah Mtukufu isemayo: "Na katika mbingu kuna riziki zenu, na yale mliyoahidiwa." ***[Qur'an, 51:22].***

Anas bin Malik (Allah amridhie) amesema, siku alipowasili Abdulrahman bin Auf katika mji wa Madina, Mtume (rehema na amani zimshukie) alimuunganisha na Sa'ad bin ar–Rabi (Allah amridhie) wakawa ndugu. Sa'ad akamwambia Abdulrahman: "Njoo nikugawie mali yangu nusu kwa nusu. Mimi nina wake wawili, nitamwacha mmoja, akimaliza eda yake umuoe." Abdulrahman akasema: "Mwenyezi Mungu akubariki katika familia yako na mali yako, nionesheni lilipo soko." Wakamuonesha soko, akarudi siku hiyo akiwa na maziwa kidogo yaliyokaushwa pamoja na samli. Vitu vyote hivyo alivipata katika biashara. Baadae Mtume alimwona Abdulrahman akiwa na athari ya rangi ya manjano (manukato ya wanawake), akamuuliza, "Kuna nini?" Akasema: "Nimeoa mwanamke miongoni mwa Answar." Mtume akamuuliza: "Umempa mahari kiasi gani?" Akasema: "Uzito wa kokwa moja (ya dhahabu)." ***[Imenukuliwa na Bukhari na Muslim]."***

## \Mafundisho ya tukio hili

Sharia ya Kiislamu humlea muumini katika kufanya kazi na kutomtegemea mtu au kuomba omba. Katika tukio hili, tumemuona Abdulrahman bin Auf (Allab amridhie) akisimulia kuwa, alipohamia Madina Mtume aliunga undugu baina yake na Sa'ad bin ar–Rabi Al–Answariy Al–Khazrajiy, mmoja wa viongozi (Nuqaba') wa kiapo cha Aqabah.

Undugu (Mu'akhah) ni makubaliano ya watu wawili au zaidi kusaidiana na kushirikiana kana kwamba ni ndugu wa damu. Sa'ad (Allah amridhie) alimpa Abdulrahman nusu ya mali yake, na akapendekeza achague mmoja kati ya wakeze ili amuache kisha baada ya eda yake kumalizika amuoe.

Lakini Abdulrahman alikataa kwa sababu ya kumuheshimu, akasema kuwa hana haja na jambo hilo, kisha akauliza mahali lilipo soko ili akafanye biashara. Abdulrahman alioneshwa soko la Bani Qaynuqa (miongoni mwa makabila ya Wayahudi waliokuwa Madina), akaenda kulitembelea, baadae akaanza biashara ya kuuza samli na aqit (maziwa yaliyokaushwa) hadi akapata mali.

Mtume alipoona Abdulrahman amejipaka manukato alimuuliza: "Je, umeoa?" Akajibu: "Ndiyo." Mtume akamuuliza: "(Umemuoa) nani?" Akasema: "Miongoni mwa wanawake wa Kianswari." Alipoulizwa kuhusu mahari alisema amempa mahari yenye uzito wa kokwa moja ya dhahabu (takriban dirhamu tatu na thuluthi). Kisha Mtume akamuamuru afanye walima (sherehe ya harusi) hata kama ana kondoo mmoja.

## Utu na heshima vipo katika kipato halali

Utu na heshima ya muumini havipo katika cheo au umaarufu, bali katika kumridhisha Allah na kutafuta riziki ya halali. Kila mtu ana kipaji alichopewa na Allah, na kadri anavyopenda kazi yake ndivyo anavyojinufaisha yeye binafsi na jamii nzima.

Uislamu umeinua hadhi ya kazi na ukaweka juu yake thawabu na ujira mkubwa. Miongoni mwa dalili zinazothibitisha hilo ni kuambatanishwa kwa ibada na suala zima la kufanya kazi. Allah anasema: "Si kosa kwenu kutafuta fadhila kutoka kwa Mola wenu..." [Qur'an, 2:198].

Na kutoka kwa Ibn Abbas (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) amesema, katika zama za Mtume walikuwa wanaona aibu kufanya biashara katika misimu ya Hijja kwa kuwa ni wakati wa kufanya dhikri, basi Mwenyezi Mungu akateremsha aya hii: "Si kosa kwenu kutafuta fadhila kutoka kwa Mola wenu."

Allah Mtukufu ameoanisha baina ya wale wanaojitahidi katika njia yake na wanaosafiri ardhini kutafuta fadhila zake: "Na wengine wanasafiri ardhini wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu, na wengine wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu." [Qur'an, 73:20]. Pia Allah anasema: "Yeye ndiye aliyeifanya ardhi iwe laini kwenu; basi tembeeni katika pande zake na kuleni riziki yake." [Qur'an, 67:15].

## Mitume walikuwa wachapa kazi

Pamoja na jukumu kubwa la kuwalingania watu walilopewa na Allah, Mitume na Manabii (amani ya Allah iwe juu yao) hawakuacha kuwajibika katika kutafuta kipato cha kujikimu kimaisha. Qur'an imetuhadithia maisha ya Manabii wa Allah na kazi walizofanya.

Nabii Nuhu na Zakariya (amani iwe juu yao) walikuwa mafundi seremala, Nabii Daudi alikuwa fundi chuma akitengeneza silaha na vitu vingine vyenye manufaa kwa jamii yake, na Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) aliwahi kuchunga kondoo na kufanya biashara ili kupata riziki ya halali, licha ya cheo chake kikubwa.

Kadhalika, Masahaba wa Mtume (Allah awe radhi nao) walikuwa na hamu ya kutafuta kipato cha halali kupitia biashara na kazi mbalimbali, kama tulivyoona kwa Abdurrahman bin Auf. Mtume amesema: "Hakuna mtu aliyekula chakula bora zaidi kuliko kile alichokipata kwa kazi ya mikono yake; na Nabii Daudi alikuwa anakula kwa kazi ya mikono yake." [Bukhari].

Pia, Mtume amesema: "Mmoja wenu kubeba kuni mgongoni mwake ni bora kuliko kumuomba mtu, bila kujali kama atampa au atamnyima." [Bukhari na Muslim]. Hadith hizi mbili zinathibitisha mtazamo chanya juu ya kufanya kazi. Hivyo, mkono unaofanya kazi na kupata riziki ya halali ndiyo mnyenyekevu na unaojisitiri dhidi ya kuwaomba watu. Mwenyezi Mungu ametufungulia milango mingi ya ajira, vyuo, taasisi na shule zinazofundisha fani nyingi zenye manufaa, kama vile kompyuta, uhandisi wa umeme, ujenzi, mekanika, useremala, uhunzi, n.k.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA




# Dhana: sumu inayovuruga mahusiano ya kifamilia

Mara nyingi dhana huingia katika maisha ya familia ikiwa imejificha nyuma ya sura ya busara. Mtu hujiambia, "Najaribu kuwa makini." Lakini kilicho chini ya kauli hizi, mara nyingi, si tahadhari bali hofu, majeraha ya zamani, au uzoefu mbaya ambao haujaponywa. Hapo ndipo dhana hubadilika kutoka kinga kuwa silaha inayojeruhi mahusiano ya karibu zaidi.

Tofauti na makosa mengine ya wazi, dhana huanza ndani ya nafsi. Haionekani, haisikiki, lakini athari zake hujitokeza katika sauti ya baridi, ukimya wa makusudi, au adhabu zisizoelezeka. Ndani ya familia, ambako watu wanapaswa kuwa salama kihisia, dhana hugeuza nyumba kuwa uwanja wa tahadhari na mashaka.

Allah (Subḥānahu wa Taḥālā) anasema wazi: "Enyi mlioamini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi...." [Quran, 49: 12].

Aya hii inaanza kwa wito wa imani, ikionyesha kuwa kuacha dhana si suala la adabu tu, bali ni sehemu ya ulinzi wa imani na ucha-Mungu, hasa ndani ya nyumba ambako mahusiano yanapaswa kujengwa juu ya uaminifu.

## Dhana kama zao la majeraha ya zamani

Katika familia, dhana mara nyingi hutokana na majeraha ya kihisia ambayo hayajaponywa. Mzazi aliyewahi kudhulumiwa anaweza kuanza kuona hatari kila mahali, hata pale ambapo hakuna ushahidi. Mwenzi aliyewahi kuumizwa hujenga kuta za mashaka ili asiumizwe tena.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, tatizo hapa si tahadhari, bali ni kuruhusu hofu ichukue nafasi ya tawakkul (kumtegemea Allah) na mawasiliano ya wazi. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alionya: "Jihadharini na dhana, kwani dhana ni uongo kuliko maneno yote." [Bukhari na Muslim]

Hadith hii ina uzito mkubwa katika malezi, kwa sababu mzazi au mwenzi anapojenga hukumu ya ndani bila dalili, hujenga uongo unaoonekana kama ukweli moyoni mwake.

## Dhana na ukimya unaovunja nyumba

Si kila dhana hujitokeza kwa maneno makali. Mara nyingi hujificha katika ukimya. Mtu anapochagua kunyamaza badala ya kuuliza, huacha nafasi ya mawazo kujaza pengo. Mawazo hayo kwa kawaida huelekea upande mbaya.

Kadri ukimya unavyoendelea, ndivyo simulizi ya ndani inavyokuwa "ukweli" mpya. Hii ndiyo sababu familia nyingi huvunjika bila ugomvi mkubwa; zilivunjwa na mambo yasiyosemwa.

Kwa watoto, ukimya huu ni hatari zaidi. Mtoto anapohisi mabadiliko ya hisia kwa mzazi bila maelezo, hujilaumu. Anaweza kudhani hakubaliki au hafai, ilhali chanzo ni dhana ya mzazi ambayo haijawahi kusemwa wala kufafanuliwa.

Ukimya huu huua mawasiliano na hufanya kila upande aishi na tafsiri yake binafsi. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa mfano wa kuondoa mashaka kabla hayajakua. Katika tukio maarufu alipokuwa akitembea na mke wake Ḥafiyyah (Allah amridhie), aliwaambia Maswahaba waliompita: "Huyu ni Ḥafiyyah, mke wangu." Kisha akasema: "Shetani hupita ndani ya mwanaadamu kama damu, nami niliogopa akatie dhana katika nyoyo zenu." [Bukhari na Muslim].

## Dhana katika zama za kidijitali

Katika familia za leo, dhana imepata uwanja mpya: simu na mitandao ya kijamii. Kuona ujumbe, picha au hali (status) bila muktadha kamili na ujumbe usiojibiwa huzaa tafsiri zisizo sahihi. Mzazi anaweza kudhani mtoto ana tabia mbaya kwa picha moja, au mwenzi akahukumu uaminifu kwa kuona jina au emoji. Teknolojia imeharakisha dhana, lakini haijatoa hekima ya kuzidhibiti.

Uislamu unatufundisha kuthibitisha habari kabla ya kuzihukumu: "Enyi mlioamini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyoyatenda." [49:6].

## Kujenga utamaduni wa kuuliza kwa adabu

Familia imara hujengwa juu ya ujasiri wa kuuliza maswali magumu kwa upole. Kuuliza hakumaanishi kushambulia; ni ishara ya kuthamini uhusiano. Mzazi anayemuuliza mtoto, "Nisaidie nielewe kilichotokea," anafungua mlango wa mafunzo. Mwenzi anayesema, "Nilihisi hivi, unaweza kunieleza?" anajenga daraja badala ya ukuta.

Ni muhimu pia kujifunza kuchelewesha majibu. Hisia zinapopanda, kusubiri kabla ya kutoa hitimisho huzuia dhana kugeuka kuwa uamuzi. Familia inayojenga utamaduni wa kuuliza badala ya kudhani hujenga mazingira ya amani na usalama wa kihisia, hasa kwa watoto.

## Ponyeni chanzo, si dalili

Ili dhana ipungue, familia inahitaji kushughulikia chanzo chake: hofu, majeraha ya zamani na ukosefu wa mawasiliano. Mazungumzo ya mara kwa mara ya kihisia, kusamehe, na kujenga uaminifu hatua kwa hatua ni tiba ya muda mrefu. Watoto wanapofundishwa kutaja hisia zao kwa maneno, wanajifunza kuwa dhana si njia pekee ya kuelewa dunia.

# MAKALA SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS




# Kwa nini tunachukia?

**Chuki mara nyingi huchukuliwa kama hisia ya kawaida, sawa na furaha, hofu au huzuni. Tunaposikia mtu akisema "namchukia" au "nachukia hali hii," tunaamini kuwa ni hisia ya moja kwa moja inayotokea bila hiari.**

**Hata hivyo, utafiti wa kisaikolojia unaonyesha huo sio ukweli wote, chuki si hisia ya asili, bali ni tabia tunayojifunza. Hujengwa polepole kupitia hofu, hasira, msongo wa mawazo na mazingira ya kijamii yanayotuzunguka.**

**Kwa mujibu wa uchambuzi wa mwanasaikolojia Sam Goldstein, chuki haipo peke yake. Huwezi "kuhisi" chuki bila kwanza kupitia hofu, maumivu, hasira au hisia ya kutishiwa. Kwa maana hiyo, chuki ni mwitikio wa kujilinda, si msukumo wa kiasili wa ubongo wa binadamu.**

## Chuki kama zao la hofu

Hofu ni chanzo kikuu cha chuki. Binadamu huogopa kile asichokielewa au anachokiona kama tishio. Tofauti za rangi, dini, utamaduni au mtazamo wa kisiasa huweza kuonekana kama hatari, hata bila ushahidi. Ubongo unapokosa taarifa sahihi, hujaza pengo kwa dhana mbaya. Hatua hii ya kisaikolojia ndiyo chanzo cha chuki nyingi za kijamii kama ubaguzi wa rangi au chuki dhidi ya wageni.

## Msongo wa mawazo na hitaji la kulaumu

Wakati mtu anapokuwa chini ya msongo mkubwa wa mawazo—kiuchumi, kihisia au kijamii—huanza kutafuta pa kuelekeza hasira yake. Chuki hutoa njia rahisi ya kutoa mzigo wa ndani. Badala ya kukabiliana na chanzo halisi cha matatizo, mtu humlaumu mtu au kundi fulani. Hii ndiyo sababu katika nyakati za misukosuko ya kijamii au kiuchumi, chuki huongezeka haraka.

## "Sisi dhidi yao"

Kisaikolojia, binadamu ni viumbe wa makundi. Tunajitambulisha kwa "sisi" na mara nyingi huwatenganisha wengine kama "wao." Mtazamo huu wa kikundi huimarisha mshikamano wa ndani, lakini pia huzaa chuki kwa walio nje ya kundi. Kadiri mtu anavyoamini kuwa kundi lake ni bora au sahihi zaidi, ndivyo inavyokuwa rahisi kuhalalisha chuki, ubaguzi au hata ukatili dhidi ya wengine.

## 'Kudogosha' uzito wa chuki

Katika jamii ya kisasa, neno "chuki" limerahisishwa. Watu husema "nachukia Jumatatu" au "nachukia foleni" wakimaanisha kero ndogo.

Matumizi haya mepesi hufanya chuki ionekane kama jambo la kawaida na lisiloepukika. Kisaikolojia, hili hupunguza uzito wa neno na kuficha hatari yake halisi inapogeuka kuwa chuki dhidi ya watu au makundi.

## Mtandao kama njia ya kukuza chuki

Mitandao ya kijamii imeongeza kasi ya kujifunza chuki. Mazingira ya mtandaoni huruhusu watu kusema maneno makali bila uwajibikaji wa moja kwa moja. Aidha, "vyumba vya mwangwi" (echo chambers) huwafanya watu wasikie maoni yanayofanana na yao pekee, jambo linalothibitisha chuki walizonazo badala ya kuzipinga. Habari potofu na vichwa vya habari vya kuchochea hisia huimarisha zaidi mzunguko huu.

## Gharama ya kisaikolojia ya chuki

Chuki haimuumizi anayelengwa pekee; humuangamiza pia aliye nayo. Tafiti zinaonyesha kuwa watu wanaoshikilia chuki wana viwango vya juu vya msongo wa mawazo, wasiwasi na matatizo ya kiafya. Kisaikolojia, chuki hutumia nguvu nyingi za kiakili, hupotosha mtazamo wa uhalisia na humfanya mtu aishi katika hali ya tahadhari na hasira ya kudumu.

## Kuvunja mzunguko wa chuki

Kwa kuwa chuki ni tabia iliyojifunza, inawezekana pia kuiacha. Hatua ya kwanza ni ufahamu: kutambua kuwa hisia tunazoita chuki mara nyingi ni hofu au hasira isiyotambuliwa. Elimu na kukutana na watu tofauti hupunguza hofu na kubomoa dhana potofu. Kisaikolojia, uzoefu halisi huwa na nguvu zaidi kuliko simulizi tulizojifunza.

Huruma (empathy) ni tiba muhimu. Mtu anapojifunza kuona ulimwengu kwa macho ya mwingine, ubongo hupunguza majibu ya uadui. Mazungumzo ya wazi, hata juu ya mada ngumu, husaidia kuvunja ukuta wa "sisi dhidi yao."

Aidha, kujifunza kudhibiti hisia—kupitia tafakuri, ushauri wa kisaikolojia au mbinu za kupunguza msongo—hupunguza uwezekano wa hasira kugeuka chuki.

Kisaikolojia, chuki si hatima wala silika; ni mwelekeo unaojengwa. Ingawa huonekana kumpa mtu nguvu ya muda mfupi, kwa hakika humtenga, humchosha na humharibu. Njia mbadala ya chuki si lazima iwe upendo wa ghafla, bali ni udadisi, kusikiliza na utayari wa kujifunza. Tunapochagua kuelewa badala ya kuhukumu, tunavunja mzunguko wa chuki na kujijengea afya bora ya akili na jamii yenye mshikamano zaidi.



# Sifa ya chapa, kudumu katika ubora ni mtaji wa kimkakati katika biashara

**Katika ulimwengu wa biashara wa leo unaobadilika kwa kasi na uliojaa ushindani mkali, sifa ya chapa (brand reputation) na kudumu katika ubora (consistency in quality) si anasa, bali ni nguzo kuu za mafanikio ya muda mrefu. Biashara nyingi hutambua umuhimu wa sifa njema pale tu inapoharibika—wakati wateja wameondoka, imani imetikisika, na kurejesha uaminifu kunakuwa gharama kubwa zaidi kuliko kuujenga tangu mwanzo.**

**Heshima ya chapa ni mtazamo wa pamoja unaojengwa katika akili za wateja, wafanyakazi, wawekezaji na jamii kwa ujumla. Ingawa ni dhana isiyoonekana, athari zake ni halisi sana. Chapa yenye heshima huaminika, hupendwa, na hupewa nafasi ya kwanza katika maamuzi ya ununuzi. Kinyume chake, chapa yenye sifa mbaya hupoteza wateja, hupata ugumu wa kuvutia wafanyakazi bora, na mara nyingi hulazimika kushindana kwa bei badala ya thamani.**

## Kwa nini sifa ya chapa ni muhimu

Kwa upande wa wateja, sifa ya chapa hufanya kazi kama njia ya mkato ya kufanya maamuzi. Katika soko lililojaa chaguo nyingi, mteja hutumia sifa ya chapa kuamua haraka kama bidhaa au huduma fulani inafaa kuaminiwa. Biashara yenye jina zuri huonekana kuwa salama, thabiti na yenye ubora unaotabirika.

Kwa upande wa biashara, heshima ni mali isiyoandikwa kwenye mizania lakini yenye thamani kubwa. Chapa inayoheshimika huvutia wawekezaji, hushawishi wateja kulipa bei ya juu zaidi, na hujenga uaminifu wa muda mrefu. Aidha, biashara zenye heshima nzuri huwa na uwezo mkubwa wa kustahimili misukosuko ya soko na migogoro ya muda mfupi.

## Kudumu katika ubora: msingi wa sifa ya chapa

Heshima ya chapa haijengwi kwa kampeni za matangazo pekee, bali kwa uthabiti wa uzoefu wa mteja. Kudumu katika ubora kunamaanisha mteja kupata kiwango kilekile cha huduma au bidhaa kila anaposhirikiana na chapa husika. Iwe ni duka dogo la mtaa au kampuni kubwa ya kimataifa, kutotabirika kwa ubora huvunja imani haraka.

Biashara zinazobadilisha rangi, ujumbe, viwango vya huduma au ahadi za chapa mara kwa mara huonekana kama zisizo na mwelekeo. Kisaikolojia, wateja huamini zaidi kile wanachokizoea. Ndiyo maana chapa imara hujulikana kwa sauti moja, taswira moja na viwango visivyobadilika kirahisi.

## Uongozi unachangia sifa ya chapa

Viongozi wa biashara wana nafasi kubwa katika kujenga au kuharibu sifa ya chapa. Maamuzi yao, kauli zao na mienendo yao huakisi moja kwa moja chapa wanayoiongoza. Kiongozi anayejali maslahi ya muda mfupi au umaarufu binafsi anaweza kuhatarisha afya ya muda mrefu ya chapa.

Uongozi wenye maadili, uwazi na uthabiti hujenga heshima ya kudumu. Wakati viongozi wanapoweka mbele maslahi ya jamii, wafanyakazi na mazingira—sambamba na faida—chapa huonekana kuwa na dhamira ya kweli, si biashara ya faida pekee.

## Heshima ya chapa wakati wa migogoro

Heshima ni "ngumu kuondoka." Ikiharibika, huomba juhudi kubwa kuirejesha. Ndiyo maana katika nyakati za migogoro, biashara zinapaswa kuchukua hatua za haraka na za uwazi. Kukiri kosa, kurekebisha tatizo na kuonyesha mabadiliko kwa vitendo ni hatua muhimu katika kurejesha imani.

Biashara zinazojaribu kuficha ukweli au kulaumu wengine mara nyingi huongeza hasara ya heshima. Kinyume chake, zile zinazoonyesha uwajibikaji huweza hata kutoka kwenye mgogoro zikiwa na uaminifu mkubwa zaidi kuliko awali.

## Uthabiti, wateja waaminifu na faida

Utafiti wa masoko unaonyesha kuwa kupata mteja mpya ni gharama kubwa zaidi kuliko kumhifadhi mteja wa zamani. Kudumu katika ubora na ujumbe wa chapa hujenga uaminifu wa wateja, ambao huzaa mapato ya muda mrefu. Wateja waaminifu si wanunuzi tu; huwa mabalozi wa chapa kupitia mapendekezo ya mdomo kwa mdomo. Biashara yenye sifa nzuri pia huonekana kuwa ya thamani ya juu. Wateja huwa tayari kulipa zaidi kwa chapa wanayoamini, jambo linaloongeza faida bila kuongeza gharama kubwa za uendeshaji.

## Kubadilika bila kupoteza utambulisho

Ingawa uthabiti ni muhimu, biashara pia zinahitaji kubadilika kulingana na mabadiliko ya soko, teknolojia na matarajio ya wateja. Changamoto ni kubadilika bila kupoteza kiini cha chapa. Biashara zilizofanikiwa huweza kuanzisha bidhaa mpya au kuingia masoko mapya huku zikidumisha maadili, sauti na ubora unaotambulika.